SportPesa
TZS. 686,934,380
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



KESI YA SABAYA
**Shahidi** adai kuidhinisha kutolewa mil.90/- benki
UKURASA 5



**Lukaku aanza mazoezi Chelsea**
UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Novemba 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580767

www.ippmedia.com
twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Warioba atema cheche rushwa kwenye uchaguzi

• **Afichua** namna viongozi wanavyoikwaza TAKUKURU...*Uk.2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**WADAU HABARI WAIPA MAPENDEKEZO SERIKALI**

WADAU wa Habari wamewasilisha serikalini mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazogusa sekta...

## Kijana alazwa ICU tuhuma kichapo cha polisi

UKURASA 3











Picha tofauti za tukio la ajali ya magari manane baada ya kugongana kwenye barabara kuu ya Segera-Chalinze katika Kijiji cha Kwedibomba, Kata ya Kwedibomba, Tarafa ya Mzundu, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ajali ya magari manane ilivyojeruhi watu 16

UKURASA 3

**MICHEZO** **PABLO ADUWAZA KWA UFUNDI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (katikati) na wenzake wakitoka katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza mashtaka yanayowakabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Warioba atema cheche rushwa kwenye uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
NGORONGORO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesema tatizo la rushwa kwenye siasa hususani wakati wa uchaguzi linashindwa kukomeshwa nchini kwa sababu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) imebaki kuwa chombo cha kupewa maagizo na viongozi, ambao baadhi yao ndio wanaojihusisha na rushwa.

Alisema hayo juzi katika mahojiano na Kipindi cha Dakika 45, kinachorushwa na runinga ya ITV kuhusu tathmini ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika mambo mbalimbali yaliyofanyika.

Jaji Warioba alisema kwenye siasa rushwa inaonekana waziwazi ambapo mtu anayetaka uongozi siku hizi analazimika kutumia fedha na bila fedha huwezi kupata uongozi, jambo ambalo linafanya rushwa iendelee kuenea.

Alisema TAKUKURU ilianzishwa kwa lengo la kupambana na rushwa na hasa rushwa kubwa, na kwamba huko nyuma chombo hicho kilifanya kazi nzuri, lakini hivi sasa kimekuwa kikosi cha kupewa amri na viongozi.

"Ni wasiwasi mkubwa kwa jinsi ambavyo TAKUKURU inatumika, imekuwa kama Jeshi la Polisi, inapewa maagizo wakati huko nyuma kilikuwa kikosi ambacho kinafanya kazi yake bila kuingiliwa ndio, maana ilikuwa na uwezo hata kuchunguza mambo yanayohusu wakubwa," alisema na kuongeza:

"Lakini hivi sasa kimekuwa kikosi cha kupewa amri, sasa ni kama kipo chini ya viongozi, ni vigumu sana kikosi hicho kuwachunguza viongozi, na ndio maana rushwa na siasa inaendelea na hatuoni hatua zikichukuliwa kwa sababu ambao wangeweza kuchukua hatua ni TAKUKURU, lakini wanapewa maagizo na viongozi."

Alisema inashangaza kuona hivi sasa kila mmoja anatoa maagizo kwa TAKUKURU na kuifanya taasisi kuwa kama ipo chini ya wakubwa na inapofika wakati wa uchaguzi viongozi hao hao wanakuja na fedha nyingi sana.

Warioba alisema sheria ya kuzuia rushwa inataka lazima uonyeshe fedha ulizonazo na chanzo chake, lakini suala hilo halitiliwi maanani wakati wa uchaguzi.

"Ukiona mishahara wanayoipata haiwezekani wakawa na fedha nyingi lazima kuna ubadhirifu, wizi umefanyika katika taasisi na hili kwa kuwa lipo kwa uongozi inakuwa kazi ngumu kulidhibiti," alisema.

Alisema ifike wakati viongozi wakubali kuwa kuna tatizo la rushwa na lipo ndani ya uongozi, hivyo kinachotakiwa ni kuweka utaratibu kushughulikia rushwa ndani ya viongozi na viongozi wenyewe wakiamua kulikomesha litafanikiwa.

Warioba alisema serikali ya awamu ya tano na sasa ya sita mwelekeo wake ulikuwa mzuri wa kupambana na rushwa, ubadhirifu na kulinda rasilimali za taifa, lakini bado rushwa ndogo kwenye huduma kama afya, umeme na ardhi zipo kama kawaida.

**MATABAKA**

Akizungumzia kuhusu matabaka, alisema mambo haya yanakuja kwa kasi nchini hasa kwa upande wa siasa.

"Limekuja tabaka la waheshimiwa na tabaka la watu wa kawaida ambapo waheshimiwa viongozi wanaanza kuonekana kama tabaka fulani," alisema.

Warioba alisema ukienda katika mikutano kunakuwa na misululu mirefu ya utambulisho na wanaotambulishwa ni viongozi na watu wengine wananuna wasipoitwa waheshimiwa.

Aliongeza kuwa huko nyuma ulikuwa ukipata nafasi ndio heshima yako, kama mtu amechaguliwa rais hiyo ni heshima au waziri, mbunge na diwani hiyo ni heshima, lakini hivi sasa inaonekana kama hiyo haitoshi, lazima tuongezee mambo mengine.

"Juzi juzi hapa Spika alizungumza kwenye Bunge kuwa anakerwa sana na hawa wanasheria wanaojiita wasomi, nadhani alichukua mfano mbaya... mimi nadhani ni kwa viongozi wanapenda sana kuonekana wao ni tofauti, na wengine wanajitambulisha mimi mheshimiwa fulani," alisema.

Warioba alisema kufanya hivyo ni kama unataka kujenga kundi la waheshimiwa wakati utamaduni huo huko nyuma haukuwapo.

## KESI YA MBOWE

# Jaji aomba muda uamuzi wa 'diary'

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa malumbano ya kisheria kuhusu maombi ya kuondolewa kwa shahidi wa Jamhuri aliyekutwa na 'diary' kizimbani wakati akitoa ushahidi.

Uamuzi huo katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu ulitakiwa kutolewa jana na Jaji Joackim Tiganga, lakini uliahirishwa, baada ya jaji kuomba muda zaidi wa kuandaa.

"Niliahirisha shauri nikasema nitatoa uamuzi leo (jana), lakini kutokana na wingi wa hoja, naomba muda zaidi, naomba radhi kwa ahirisho hili ambalo hatukulitarajia wote," alisema.

Alisema uamuzi huo atautoa leo kisha, aliahirisha kesi na kuamuru washtakiwa waendelee kukaa mahabusu hadi leo.

Mawakili wa pande zote mbili waliingia katika malumbano ya kisheria baada ya jopo la mawakili wa utetezi kuwasilisha hoja za kutaka shahidi wa pili kwenye kesi ndogo, Koplo Msemwa kuondolewa na ushahidi wake uondolewe kwenye kumbukumbu za Mahakama kwa sababu hafai.

Wakili Jeremiah Mtobesya akiwasilisha hoja alidai Novemba 12, mwaka huu, shahidi akiwa kizimbani anatoa ushahidi kwenye kesi ndogo, alionwa akiwa na 'diary', simu na kalamu.

Anadai wakati Wakili Peter Kibatala anatoa hoja, diary hiyo ilikuwa wazi na baada ya kuwasilisha hoja Mahakama iliona busara kumrejeshea simu na kubakia na diary. Alidai suala hilo limejitokeza kati kati ya mwenendo wa shauri, shahidi aliyekuwa kizimbani anaruhusiwa kuwa na nyaraka yoyote endapo ataruhusiwa na Mahakama na ruhusa itatoka pale anapotakiwa kufanya rejea. Mtobesya alidai ikitokea kuna umuhimu wa kiambatanisho au nyaraka kuingia mahakamani basi utaratibu utafuatwa na utaratibu uliotajwa kwenye sheria ya mwaka 2019 sura ya 200 ni shahidi kuomba ruhusa kwa Mahakama.

Alidai taratibu lazima zifatwe ili washtakiwa wapate haki zao wakati wa maswali ya dodoso, ikitokea shahidi kafanya kwa kificho inamnyima haki mshtakiwa ya kujua shahidi alirejea kwenye nini.

Mtobesya alidai mahakama hiyo ina uwezo wa kumwondoa shahidi na msimamo wa upande wa utetezi kuwa shahidi alikuwa akitoa majibu kwenye diary wakati anatoa ushahidi.

Akiwasilisha hoja Wakili Peter Kibatala alidai ni misingi ya kisheria kwamba hairuhusiwi kuwa na nyaraka kizimbani, isipokuwa kifaa kazi cha uapishaji.

"Kwa mujibu wa sheria, shahidi ambaye ameingia na nyaraka isiyoruhusiwa sio shahidi sahihi, kwanza kwa kuingia nayo na pili kwa kushindwa kuomba ruhusa.

"Kama kumwondoa shahidi ni hatua kali basi turuhusu tuone alikuwa anaandika nini humo, majina ya askari aliokuwa anawataja, tarehe alizokuwa anataja au taarifa aliyokuwa anatoa,"alidai Kibatala.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, akijibu hoja za utetezi alidai msimamo wao hawakubaliani na misingi ya hoja za upande wa utetezi, lakini hawakubaliani na maombi yaliyowasilishwa.

"Wakati shahidi anaongozwa kuanzia maapisho mpaka anatoa ushahidi wake, Mahakama ilikuwa ikimtazama, hakuna hata mmoja wetu aliyesimama kwamba shahidi alikuwa akiongozwa na kuna vitu alikuwa anasoma, kuvirejea, hiyo hoja haikuletwa," alidai Chavula.

Alidai hakuna mahali ilionyesha kuwa shahidi haelewi na majibu aliyokuwa anatoa hayana mahusiano mbele ya mahakama na pili hakuna mahali ilipoelezwa kuwa wakati anahojiwa na mwendesha mashtaka alishindwa kujibu maswali. Wakili wa Serikali, Mwandamizi, Pius Hillar, akiongezea hoja alidai hoja za mawakili wa utetezi hazipo sawasawa na Mahakama haijaelekezwa kwa kujitosheleza.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi ikiwamo kumdhuru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

HABARI KITAIFA

# Kijana alazwa ICU tuhuma za kichapo cha polisi

**Na Romana Mallya**

NI unyama! Ndivyo unavyoweza kuuita. Hii ni baada ya mkazi wa Goba mkoani Dar es Salaam, Issa Kassim (20), ambaye amelazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), kudaiwa kupigwa na kujeruhiwa na askari wa Jeshi la Polisi wa kituo cha Goba.

Tukio hilo ambalo linadaiwa kutokea Novemba 10, mwaka huu, kituoni hapo baada ya kijana huyo kukamatwa na askari polisi kwa madai ya wizi wa luninga, tayari Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limeshafungua jalada la uchunguzi huku likiita malalamiko ya ndugu ni mazito.

"Kijana huyu inadaiwa alikamatwa Novemba 10, kwa tuhuma za wizi wa luninga na baadaye kupigwa huku ikidaiwa ndugu zake walikuwa wakiombwa rushwa ili aachiwe.

"Malalamiko hayo ni mazito hivyo Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limeshafungua jalada la uchunguzi na mifumo ya kisheria itatumika ili kupata ukweli wa jambo hili na ikibainika ni kweli hatua za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahusika. Uchunguzi umeshaanza." Kamanda Muliro alisema.

Taarifa ya ndugu iliyosambaa mtandaoni jana ambayo ndiyo iliyoibua kuwapo kwa tukio hilo, ilifichua madai ya ndugu yao kupigwa na askari hadi kulazwa ICU na kudai polisi kutaka fedha ili wamuachie.

Ndugu hao walibainisha kwamba madaktari wamewaeleza kuwa kupona kwake utakuwa muujiza wa Mungu.

Sehemu ya taarifa hiyo ilidai kijana huyo alikamatwa na polisi nyumbani kwao Goba baada ya kuuziwa runinga ya wizi, tukio ambalo ndugu hao walidai mtuhumiwa alikana kulitenda.

"Baada ya kumkamata waliondoka naye wakidai wanampeleka kituo cha polisi Goba, lakini kabla ya kufika huko kituoni walimuomba awapigie simu ndugu zake waweze kumuokoa.

"Mtuhumiwa alipiga simu kwa mama yake akazungumza na mmoja wa polisi hao (wanamtaja kwa jina moja) wa Kituo cha Polisi Goba, katika mazungumzo na mama wa mtuhumiwa huyo, alimuomba atume Sh. 800,000 ili kijana wake waliyemshikilia kwa tuhuma ya kununua runinga ya wizi waweze kumuachia" ilidai taarifa hiyo.

Ndugu hao walidai kuwa mama wa mtuhumiwa aliomba apunguziwe dau hilo, badala ya Sh. 800, 000 atume Sh. 500, 000, ombi ambalo polisi hao walilikubali ingawa mtuhumiwa baada ya kusikia maongezi hayo alimzuia mzazi wake kufanya hivyo kwani hajatenda kosa, anasingiziwa.

"Baada ya mtuhumiwa huyo kuzuia fedha kutumwa, polisi hao wakiongozwa na (wanawataja polisi mawili), walimpiga sana, hasa maeneo ya kichwa kwa kutumia nyaya ngumu wakidai ni jeuri anazuia wao wasitumiwe fedha ili aachiwe," ilidai.

Taarifa hiyo ilidai kuwa polisi walimtaka apige simu kwa ndugu mwingine ambapo safari hii alipigiwa binamu wa mtuhumiwa, Tusekile Shadrack, na alipoomba namba itakayopokea ndipo polisi wakamtaka atume kwa Kassim au kwa wakala ingawa nalo halikufanikiwa.

Taarifa hiyo ilidai, siku iliyofuata (Novemba 11), asubuhi, mmoja wa askari hao walimpigia simu mama wa mtuhumiwa wakimtaka afike Hospitali ya Mwananyamala kwani hali ya mwanaye ni mbaya na ndugu walimkuta akizungumza kwa shida na kutokana na hali yake alihamishiwa Muhimbili.

**MOI WAZUNGUMZA**

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, aliithibitishia NIPASHE jana kuwa majeruhi huyo amelazwa hapo na yupo chini ya uangalizi maalum.

**KAULI YA SAMIA KWA POLISI**

Agosti 25, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, alimuagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP, Simon Sirro, kuliangalia upya suala la uwapo wa matukio ya watu kufia mikononi mwa polisi na waangalie namna mpya ya kukomesha matumizi makubwa ya nguvu kwa raia.

Kauli hiyo aliitoa wakati akifungua kikao kazi cha maofisa wakuu waandamizi wa Jeshi la Polisi, makamanda na vikosi na kuwaeleza kuwa, "Mtumiwa anapokufa mikononi kwako, askari wa polisi umemchukua huko umeshamchapa virungu vya kutosha binadamu sisi tuko wa afya za tofauti tofauti.

"Mwingine hata uchape vipi bado yuko ngangari mwingine vifimbo viwili tu tayari kashafariki mbele ya haki, kesi za watu kufa kwenye vituo vya polisi havileti sifa nzuri." Rais Samia alisema siku hiyo.

**LHRC WAFUNGUKA**

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amelitaka Jeshi la Polisi kutenda haki kuhusiana na tukio hilo kwa sababu hakuna sehemu yoyote ya sheria inasema polisi wampige mtu.

"Utaratibu wa makosa ya jinai ni kwamba mtu kama yupo ndani yupo chini ya ulinzi hivyo tayari hana msaada na hatakiwi mtu kupigwa akiwa kituo cha polisi, hata kama anafanya fujo atatulizwa kiutalaam. Ukiangalia ripoti yetu ya haki za binadamu iliyopita, matukio ya watu kupigwa vituo vya polisi na wengine wanakufa ndani ya vituo hivi yapo."



Naibu Waziri Mkuu wa Singapore, Heng Swee Keat (kulia), akimwonyesha Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, mandhari pamoja na namna nchi ya Singapore ilivyopangiliwa katika ujenzi wa majengo na miundombinu katika eneo la Shenton Way nchini jana. **PICHA: OMR**

# Ajali magari manane ilivyojeruhi 16

**Na Mwandishi Wetu**

MAGARI manane yakiwamo ya Jeshi la Polisi yamegongana na kujeruhi watu 16.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Usalama barabarani Mkoa wa Tanga, Leopard Fungu, tukio hilo lilitokea Jumapili jioni barabara ya Segera-Chalinze katika kijiji cha Kwadiloma kata ya Kwedibomba, Tarafa ya Mzundu, Wilaya ya Handeni Mkoa wa Tanga.

Taarifa yake ilisema gari namba T. 131 DVU aina ya HOW lenye tela namba T.329 DMR lililokuwa likiendeshwa na Saimon Kristo (36), mkazi wa Kibaha Pwani likitokea Kabuku kuelekea Chalinze lilipojaribu kulipita gari la mbele yake mahali pasipo ruhusiwa ndipo mbele yake likatokea gari lingine.

"Gari hilo lingine lilikuwa likitokea Chalinze kuelekea Kabuku lenye namba PT. 4036 Ashok Leyland, mali ya Jeshi la Polisi Tanzania lililokuwa likiendeshwa na H.3637 CPL Juma Chuo cha Polisi CCP Kilimanjaro.

"Dereva huyo wa gari la Polisi naye alisimama ghafla ili kuepuka ajali na ndipo likatokea gari lingine nyuma yake lililokuwa likitokea Kabuku PT.4087 Ashok Leyland lililokuwa likiendeshwa na F.7658 CPL John Robert wa Makao Makuu Madogo ya Polisi Dar es Salaam na kugonga kwa nyuma ghafla na hapo hapo nyuma yake ikaja gari namba PT.4097 Ashok Leyland lililokuwa likiendeshwa na F.5889 CPL Kigiri wa Polisi Makao Makuu Madogo Dar es Salaam na kusimama ghafla.

"Na PT.4087 Ashok Leyland na kusababisha gari namba PT.2370 Isuzu Bus ikiendeshwa na G.6123 CPL Abel wa Chuo cha Polisi Kidatu na kugonga ubavuni gari namba PT.4087 Ashok Leyland."

Taarifa hiyo ilisema lilitokea lingine namba T.573 AYR Toyota Corolla ikiendeshwa na Amin Rasul, mkazi wa Tanga na kusimama ghafla baada ya kuona ajali na kusababisha gari namba SU 44275 GX V8 mali ya TANESCO Dar es Salaam ikiendeshwa na Juma Hassan na kuigonga kwa nyuma gari T.573 AYR Toyota Corolla.

Pia taarifa hiyo ilisema ikasababisha gari nyingine namba T 773 CND Toyota Hilux kuigonga kwa nyuma gari hiyo ya TANESCO na kusababisha majeruhi kwa watu 16 ambao walitibiwa na kuruhusiwa.

Ilisema chanzo cha ajali ni uzembe wa dereva wa gari T.131 DVU lenye tela T.329 DMR ambaye alijaribu kulipita gari iliyokuwa mbele yake pasipo kuchukuwa tahadhari na kwa sasa anashikiliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alipotafutwa jana jioni, simu yake ya kiganjani ilipokewa na msaidizi wake ambaye alisema bosi wake alikuwa kwenye kikao.

# PM akaribisha wawekezaji kutoka Uingereza

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameita wawekezaji kutoka Uingereza kuwekeza nchini hususan kwenye mwambao wa ufukwe wa Bahari ya Hindi.

Amesema eneo hilo linahitaji mtaji na teknolojia ya kisasa kuendelezwa ili kuinua uchumi wa bluu utokanao na malighafi zilizomo baharini ikiwamo nishati ya mafuta na gesi.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Jukwaa la Wafanyabiashara la Tanzania na Uingereza lililokutanisha wadau tofauti kutoka ndani na nje ya nchi katika sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji wapatao 200.

Alisema Tanzania ina mazingira bora ya uwekezaji kutokana na jiografia, rasilimali watu, usalama, amani na malighafi zilizopo ambazo zipo baharini na nchi kavu, na kwamba mwaka 2016 hadi 2020 imefanikiwa kuingia kwenye uchumi wa kati.

"Kuanzia Machi hadi Agosti mwaka huu, Tanzania imeongoza kwa viwango vya uwekezaji kwa ukanda wa Afrika Mashariki na kufikia Dola za Kimarekani bilini 2.984. mafanikio haya yamechangiwa na usimamizi mzuri wa sera za uchumi...ripoti ya dunia ya uwekezaji iliyotoka Juni mwaka huu, uwekezaji wa mwaka 2020 ulifikia dola bilioni moja," alisema Majaliwa.

Majaliwa alifafanua kwamba uhusiano wa Tanzania na Uingereza ni wa kihistoria na unaimarika wa kibiashara na fursa zipo pande zote huku akisisiza kuondolewa kwa vikwazo vya uwekezaji kwenye nchi hizo, bila kuathiri soko na ushindani.

"Tangu mwaka 1990 hadi 2021 miradi yenye thamani ya Dola bilioni tano kwenye miradi 956 katika viwanda na miradi hii imesahauliwa. Hivi karibuni tumeona uwekezaji wao kiwanda cha sukari Kilombero.

"Kuna taasisi kutoka UK ambayo tayari imetoa paundi bilioni 2.5 kwa ajili ya miradi ya mafuta na gesi...Mwingereza njoo uwekeze Tanzania imeendelea, tuna nishati ya kutosha, inaunganishwa na nchi sita zisizo na bandari," alisema Majaliwa.

Kadhalika, alisema Tanzania inahitaji uwekezaji kwenye viwanda vya dawa, uvuvi, uchakataji mazao, teknolojia ya kisasa, huku akisema kuna soko la Watanzania takribani milioni 60, ikiongezwa na lililopo nchi za Afrika Mashariki milioni 177 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) milioni 300.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, alisema kuna ongezeko la miradi iliyosajiliwa kutoka 133 mwaka jana na kufikia 164 na kwamba hivi karibuni utafanyika mradi wa bilioni tatu eneo la Kigamboni.

Mwakilishi wa Waziri Mkuu wa Uingereza, Lord Walney, alisema jukwaa hilo limelenga kukutanisha wawekezaji wa nchi mbili, akisema matarajio ni kuona Tanzania ukuaji wake unaongezeka miaka ijayo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akifurahia jambo baada ya kuzindua jengo jipya la kiwanda cha kutengeneza kemikali za ujenzi cha Sika Tanzania, Mbezi Salasala, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (kulia), Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima (wa pili kulia), Meneja Uzalishaji kiwanda hicho, Mwijarubi Shinda (wa tatu kulia) na (wa tatu kushoto) ni Meneja Mkazi Sika Tanzania, Dennis Ott. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mstaafu asotea mafao miaka 11

**Na Beatrice Shayo,** KAGERA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeshangazwa na mwalimu mstaafu kuzungushwa kupatiwa mafao yake tangu mwaka 2010, kutokana na manispaa yake kudaiwa riba na mfuko wa jamii.

Akizungumza jana mkoani Kagera wakati wa majumuisho Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alipokea taarifa kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Christine Mndeme, akieleza kile alichokibaini katika ziara yake.

Alisema mstaafu huyu amekosa mafao yake ambayo ameyafuatilia kwa muda mrefu kwa masharti halmashauri ilipe riba kwenye mfuko wa jamii.

"Mstaafu anachapwa fimbo kwa kosa ambalo hajalitenda mawasiliano yamefanyika kati ya halmashauri na Hazina matokeo yake mpaka sasa hajapatiwa mafao yake miaka 11 anaangaikia haki yake,"alisema Mndeme.

Kwa mujibu wa Mndeme, mfuko huo wa jamii wanataka walipwe riba kwa kosa ambalo lilifanywa na watu wengine kwa sababu Mkurugenzi aliyepita hawakupeleka michango kwenye mfuko huo.

"Mimi ni mtumishi hiyo adhabu inanihusu nini hilo ni kosa la mtendaji tuliangalie hili na sheria zetu zinawatesa wastaafu huyu mzee alieleza anakaribia kufa hajapatiwa mafao yake ukitaka kujua shida hii staafu kesho utajua umuhimu wa haya mafao tulifanyie kazi jambo hili," alisema Mndeme.

Chongolo baada ya kupokea taarifa hiyo alisema jambo hilo halijakaa sawa kwa mstaafu kufuatilia mafao yake tangu mwaka 2010 na kuwataka viongozi kulifuatilia kwa kina aweze kupatiwa fedha zake.

Alisema anachokifahamu mishahara ya serikali inapelekwa kwa halmashauri kwa asilimia 100 ni kwa nini mtumishi hakupelekewa fedha zake katika huo mfuko wa jamii.

"Lazima wakuu wa wilaya kufuatilia suala hilo sababu ya fedha hizo kutokwenda kulipa akiba za uzeeni za mtumishi zilikuwa ni nini," alisema Chongolo.

Aliongeza: "Kama fedha ilikuja ni kiasi gani kama ilikuwa na upungufu kwa nini na kama hapakuwa na upungufu fedha ilienda wapi? Usikute kuna mtu yupo sehemu na amependishwa cheo wakati huyu mzee anateseka hilo haliwezi kukubalika fuatilieni kizizi na kiini cha tatizo."

Chongolo alisema kama fedha ziliidhinishwa zijulikane ziliishia wapi isije ikawa kuna mtu alichepusha fedha hizo na kujinufaisha na mhusika kubaki na mateso.

## Waliotimuliwa CUF rasmi kwa msajili

**Na Sabato Kasika**

MAKADA 10 wa Chama cha Wananchi CUF), wanaodai kuvuliwa uongozi na uanachama, wamefikisha malalamiko yao kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, jijini Dodoma.

Baadhi ya makada hao ni Makamu Mwenyekiti wa CUF Zanzibar, Mussa Haji Komba, aliyekuwa mgombea mwenza wa urais 2020, Hamida Abdallah Weshi na Mjumbe wa Baraza Kuu, Abdul Kambaya.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, baada ya kufikisha malalamiko katika Ofisi ya Msajili, Kambaya alisema, kilichobaki ni kusubiri uamuzi wa ofisi hiyo ili wajue hatima yao ndani ya chama hicho.

Kambaya alitaja sababu za wao kwenda Ofisi ya Msajili kuwa ni kutaka tafsiri ya uamuzi wa kikao kilichowaondoa katika nafasi zao na ndani ya chama, kwa madai kwamba kuna ukiukwaji wa taratibu.

"Tumefikisha malalamiko kwa Msajili, kwani utaratibu uliotumika kutuvua uanachama haukufuata misingi ya Katiba ya chama ikiwamo kutotimia kwa akidi ya wajumbe na kuwapo wajumbe feki," alisema Kambaya.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa nchini, Sisthy Nyahoza, alithibitisha kupokewa kwa malalamiko ya wanachama hao, na kufafanua kuwa yatafanyiwa kisha watapewa majibu.

"Niko safari, lakini nimeshapata taarifa kuwa wamefikisha malalamiko yao, nikirudi tutakaa kuyapitia kisha watapewa majibu, hivyo uamuzi ambao utatolewa na Ofisi ya Msajili watajulishwa," alisema Nyahoza.

Nyahoza alisema, Ofisi ya Msajili ina jukumu la kulea vyama vya siasa ikiwamo kutatua migogoro inayovikabili, na kwamba ina wajibu wa kupokea malalamiko au kuingilia kati kwa lengo kuimarisha demokrasia.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, alisema ni haki yao ya kikatiba kufikisha malalamiko yao kwa msajili, ili apitie katiba ya chama hicho kisha kutoa uamuzi sahihi usio na upendeleo.

# Ndugu jela kwa mauaji

**Na Samson Chacha,** TARIME

MTU na mdogo wake wakazi wa Kitongoji cha Nyandege Kijiji cha Kegonga tarafa ya Ingwe, wilayani Tarime mkoani Mara, wamehukumiwa kifungo cha miaka mitatu na nusu kila mmoja, baada ya kukiri mauaji ya kutokukusudia.

Watu hao ni Menganyi Mwita (45) na Kerato Mwita (47) ambao walikutwa na hatia ya kumuua Ryoba Masiaga kwa kumchoma kitu chenye ncha kali kifuani baada ya kutokea ugomvi baina yao wakinywa pombe. Hukumu hiyo ya kesi namba PI 81/2021 ilitolewa juzi katika Mahakama Kuu Kanda ya Musoma na Jaji wa Mahakama hiyo, Sedekia Kisanya.

Awali, ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Mafuru Moses, kuwa tukio lilitokea Novemba 28, mwaka 2020 katika Kitongoji cha Nyandege kijiji cha Kegonga wakati watuhumiwa hao wakinywa pombe kwenye kilabu ya Ghati Ryoba, walirushiana matusi na Masiaga (marehemu ).

Kwamba waliokuwapo walijaribu kuwazuia kwa kuwatoa nje, lakini ilishindikana kwa kuwa waliendelea na Masiaga kuchomwa na kitu chenye ncha kali mara tatu kifuani na ubavuni, hivyo kufariki papo hapo baada ya kutoka na damu nyingi.

Washtakiwa hao walikiri makosa yao na kuomba kusamehewa kwa kuwa wanajutia makosa yao, na kwamba licha ya kutolewa nje ya klabu, lakini Ryoba aliwafuata na kuanzisha ugomvi upya ndipo walikasirika.

Aidha, Menganyi alidai kuwa ana mke na watoto sita huku Kerato ana mke na watoto saba, na kwamba baadhi ni wanafunzi.

Mwanasheria huyo aliiomba Mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa hao ili iwe fundisho kwa wengine. Katika hatua nyingine, Mahakama hiyo chini ya Jaji Sedekia Kisanya imemhukumu kifungo cha miaka mitatu jela, Nyamhanga Getentani mkazi wa Kijiji cha Koleri Mugumu Serengeti, kwa kosa la kumkatakata kwa mapanga na kumsababishia ulemavu wa kudumu, Juma Ntigira.

Mtuhumiwa huyo alihukumiwa kifungo hicho baada ya kukiri kutenda kosa hilo.

**Awali, ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Mafuru Moses, kuwa tukio lilitokea Novemba 28, mwaka 2020 katika Kitongoji cha Nyandege kijiji cha Kegonga wakati watuhumiwa hao wakinywa pombe kwenye kilabu ya Ghati Ryoba, walirushiana matusi na Masiaga (marehemu ).**



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (kushoto), akiteta jambo na Wakili wake, Mosses Mahuna, kabla ya kuanza kusikilizwa kwa shauri linalomkabili la uhujumu uchumi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

## KESI YA SABAYA

# Shahidi adai kuidhinisha kutolewa mil. 90/- benki

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MENEJA wa Benki ya CRDB tawi la Kwa Murombo jijini Arusha, Marry Mayoka (40), amedai kwamba akiwa kiongozi mkuu wa benki hiyo katika eneo hilo, aliidhinisha mfanyabiashara Francis Mroso kutoa fedha taslimu Sh. milioni 90 kwa mkupuo mmoja.

Pia ofisa huyo alidai baada ya kumhoji mfanyabiashara huyo kwa nini anatoa fedha hizo nyingi kwa wakati mmoja alimweleza kwamba kuna mtu anataka kumlipa na alikuwa ameambatana naye.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Tersila Gervas, shahidi huyo alidai kwamba amekuwa meneja wa benki katika tawi la kwa Murombo tangu Januari 2020.

Ole Sabaya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka matano katika mahakama hiyo, likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Ofisa huyo shahidi wa tisa wa Jamhuri, alitoa madai hayo, mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda wakati akitoa ushahidi mahakamani huko.

Shahidi huyo alidai mahakamani hapo kwamba benki imeweka utaratibu wa kulinda fedha za wateja wao, kwa kuwa na mifumo bora na imara ya ulinzi ukiwamo wa CCTV Kamera.

Kadhalika alidai, akiwa meneja wa benki amekuwa akisimamia kuhifadhiwa kwa nyaraka mbalimbali za kibenki kutokana na huduma za wateja walizopatiwa.

Pia, amekuwa akisimamia kuhifadhiwa kwa matukio yaliyorekodiwa kwenye mfumo wa CCTV Kamera kwa kipindi cha miezi sita hadi mwaka mmoja.

Shahidi huyo, alidai kwamba Januari 22, mwaka huu, majira ya saa 11 jioni akiwa katika kituo chake cha kazi, alikwenda kwa Mhasimu wa benki na alimweleza kwamba mteja wao, Francis Mroso, anataka kutoa fedha nyingi hivyo alitaka meneja huyo kwenda kuzungumza naye.

Shahidi huyo, alidai mahakamani huko kwamba baada ya kumuuliza Mhasibu huyo na alimjulisha kwamba Mroso anataka kutoa fedha benki kiasi cha Sh. milioni 90.

"Nilimfuata Mroso kumuuliza kwa nini anatoa fedha nyingi kiasi hicho kwa wakati mmoja, alinieleza kuna mtu anataka kumlipa nikamwambia kwa nini asimhamishie hela kwenye akaunti yake kama anayo na alinijibu labda mimi nikazungumze naye kama atakubali.

"Nilimfuata yule kijana kuzungumza naye kumuuliza kama ana akaunti benki na alinijibu kwamba hana, nilimshauri afungue akaunti ili tuweke fedha hizo kwa ajili ya usalama zaidi, lakini alikataa alitaka kulipwa fedha taslimu na alisema angekuja siku nyingine kufungua akaunti.

Alidai mahakamani hapo kuwa baada ya mteja huyo kutaka kulipwa fedha taslimu akiwa Meneja wa tawi aliidhinisha fedha hizo kutolewa na wahusika walipatiwa na kuwekewa kwenye boksi.

Kadhalika shahidi alidai kwamba karatasi ya kutoa fedha inathibitisha kwamba siku hiyo, Mrosso alijaza karatasi hiyo kwa ajili ya kutoa fedha, karatasi ya taarifa za kibenki (bank statement), pamoja na muhuri wa benki uliogongwa kwenye karatasi hiyo.

Hata hivyo, shahidi huyo, alidai kwamba Mei 31, mwaka huu, alipokea barua mbili kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), waliomba kupewa video za CCTV Kamera za Januari 22, Bank Statement ya Francis Mroso na karatasi ya kutoa fedha benki (withdraw statement).

"Baada ya kupewa ridhaa na ofisi yangu nilimpigia kijana yule aliyeleta barua zile anaitwa Ramadhani kwa kuwa siku ya kuleta barua nilimwomba aniachie namba yake ya simu na wakati akija alikuwa ameambatana na Johnson Kisaka kutoka TAKUKURU na nilimuita Ofisa TEHAMA wa benki Kanda ya Kaskazini, Geofrey Nnko, kuongozana nao kwenda katika chumba cha mfumo wa CCTV Kamera.

"Baada ya Geofrey Nko, kumaliza kazi hiyo kwenye mfumo kwa kutoa CCTV Kamera walikuja kwangu kunieleza kwamba wamemaliza kazi hiyo na mimi nilisaini karatasi ya kuwakabidhi kwamba nimeshawapatia," alidai shahidi huyo.

Katika hatua nyingine shahidi huyo alizitambua mahakamani nyaraka za kutoa fedha na taarifa za benki na kuiomba mahakama kuzipokea nyaraka hizo kama vielelezo vya ushahidi mahakamani.

Baada ya ombi la shahidi huyo, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alipinga kupokelewa kwa nyaraka hizo, kama vielelezo vya ushahidi akidai kwamba utaratibu wa kisheria wa kuwasilishwa mahakamani nyaraka hizo haukufuatwa.

Akijibu hoja za upande wa utetezi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, alidai kwamba, akirejea ushahidi ulitolewa na shahidi huyo, alipaswa kuonyesha usahihi wa kutolewa kwa nyaraka hizo kutoka kwenye mfumo.

Baada ya mabishano ya kisheria hakimu aliahirisha shauri hilo, hadi leo, mahakama itatoa uamuzi mdogo wa pingamizi hilo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada za kutunza mazingira ziongezeke

**WAZIRI** wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, juzi alieleza kuwa uchomaji ovyo wa misitu umekuwa moja kati ya sababu zinazochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa vyanzo vya maji nchini.

Alisema katika maeneo mengi hivi sasa kumekuwapo matukio ya uchomaji misitu ovyo hali inayotishia uharibifu wa vyanzo vya maji nchini.

Aidha, alitolea mfano kuwa Bwawa la Mindu, mkoani Morogoro, miaka ya nyuma lilitumika kama chanzo cha maji cha uhakika, lakini hivi sasa kutokana na uharibifu wa mazingira pamoja na uchomaji misitu kumekuwapo ukame mkubwa.

Pia, alisema wizara nane zimejipanga kushirikiana kushughulikia kero ya uchaguzi wa mazingira utokanao na kelele za muziki kwenye kumbi za starehe na nyumba za ibada.

Aidha, alikiri kuwa kero ya miaka yote kwa wizara hiyo ni uchafuzi wa mazingira utokanao na makelele katika kumbi za starehe pamoja na nyumba za ibada. Dunia kwa saa inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ambao umesababisha mabadiliko ya tabia nchi na sasa majira ya mvua yamebadilika, ongezeko la baridi, joto na ukame wa muda mrefu.

Mathalani, Tanzania inakabiliwa na ongezeko la joto huku mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Ruvuma ikiongoza, huku mvua zikichelewa kunyesha na kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), zinatarajiwa kuanza kunyesha mwanzoni mwa Desemba.

Ni muhimu sasa kutunza misitu kwamba sheria ndogo za kila halmashauri zifanye kazi kuliko kuendelea kuwa nazo lakini utekelezaji haupo, kasi ya ukataji miti kwa ajili ya mkaa na matumizi ya nishati inaongezeka.

Lakini, tunaona ni muhimu wananchi wakawa na nishati mbadala ili waachane na matumizi ya mkaa ambao kwa sasa ni asilimia 80 ya watumiaji, ikiwa hili litafanikiwa basi kasi ya ukataji miti itapungua.

Licha ya kuhamasisha watu kukata miti na kupanda upya ila tujiulize mti unaokatwa sasa ulipandwa miaka mingapi iliyopita na je, inakatwa mingapi kupata mkaa wa kutosha kwa ambaye amejiajiri.

Mathalani, licha ya marufuku ya serikali kukata miti, lakini kwenye barabara zote kuu ikishafika saa 11 jioni ndiyo mkaa unavyotolewa kuuzwa barabarani, na yote hiyo ni miti imeteketea.

Ni muhimu serikali ikafuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha nishati mbadala kama gesi inashuka bei, itawezesha watu wengi kutumia nishati hiyo na kuachana na kuni au mkaa ambayo inateketeza mazingira. Pia moja ya eneo korofi waziri alilizungumzia ni kelele za nyumba za ibada na sehemu za starehe, hii inaonekana ni fupa gumu lililozishinda mamlaka kwa kuwa sasa tunaona msimamizi naye anageuka kuwa mlalamikaji badala ya kutumia sheria kuchukua hatua.

Nyumba hizi za ibada na sehemu za starehe zipo kwenye maeneo yetu na ujenzi unapoanza unaonekana hata serikali za mitaa wanaona, lakini wakati mwingine nguvu ya fedha hutumika kuhakikisha biashara hiyo inaendelea.

Licha ya kutakiwa kufunga biashara hizo saa sita usiku wapo wanaoendelea, lakini huoni wakichukuliwa hatua kiasi cha wengi kushindwa kulala hasa wanafunzi na wagonjwa.

Miaka ya nyuma baadhi ya watu binafsi na taasisi walijitolea kupanda miti, na kampeni hiyo iliuongezwa na Mwenyekiti wa Kampuni za IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi, ambaye alihamasisha wananchi kupanda miti na kutunza mazingira nchini.

Hamasa hiyo ilisaidia sana kuwa na mwamko kwa watu binafsi, shule za msingi, sekondari na vyuo kupanda miti kwa wingi.

Lakini ni muhimu sheria ya kuzuia shughuli za binadamu umbali wa mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji ikaheshimiwa kwa kuwa ni kawaida shughuli za kilimo kufanyika hadi kwenye kingo za mito na kuharibu mazingira.

Bila kusimamia sheria nchi itaendelea kukabiliwa na ukame ikiwamo upungufu wa maji, na tayari tunaona mgawo wa maji unavyoshika kasi nchini na kwa kuwa umeme wetu ni wa maji basi muda siyo mrefu kiasi cha maji kitapungua kwenye mabwawa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hakuna mafanikio kupitia udanganyifu wa mitihani

Na Sabato Kasika

**KUANDAA** vijana kwa ajili ya uongozi wa taifa ni jambo la muhimu, kwa vile walio kwenye nyadhifa mbalimbali unafika muda wanastaafu na kupisha wengine kuongoza nchi.

Ni kutokana na ukweli huo, ndiyo maana kuna falsafa ya 'vijana ni taifa la kesho', ambayo inalenga kuwatayarisha kielimu, maadili na ujuzi wa nyanja nyingine nyingi, ili baadaye washike uongozi wa taifa katika nyadhifa mbalimbali.

Elimu ni miongoni mwa maandalizi muhimu kwa vijana ili hatimaye wapatikane wataalamu wa fani za kila namna watakaosukuma mbele maendeleo ya nchi na uongozi wa taifa.

Mitihani ni moja ya njia za kuwaandaa na kuwapima uelewa vijana, lakini ndani ya eneo hilo kumekuwapo na tatizo la 'kuchakachua' mitihani na kuharibu uwezo kiakili na kifikra wa viongozi bora wa baadaye.

Tatizo la kuwapo udanganyifu kwenye mitihani ya taifa kila mwaka ni hali ambayo huenda ikasababisha vijana ambao ni taifa la kesho kulinganishwa na jeshi la akiba lisilokuwa na manufaa kwa taifa lake.

Kwa mfano, mwaka jana, wanafunzi 215 walifutiwa matokeo kutokana na vitendo hivyo vya udanganyifu. Kati yao 77 ni wa darasa la nne, 63 wa kidato cha pili na 75 wa kidato cha nne ambao jumla yao ni 215.

Hizo ni takwimu za mwaka jana, lakini karibu kila mwaka taarifa za Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), hutangaza kufutwa kwa matokeo ya mitihani na kukamatwa kwa baadhi ya walimu na wanafunzi kwa kujihusisha na udanganyifu huo.

Uchakachuaji huo unachangia kupatikana viongozi wa baadaye ambao hawana uwezo, maarifa wala umuhimu kwa taifa.

Ni kutokana na ukweli kuwa ufaulu wao unatokana na njia zisizo halali na wenye mashaka.

Tunayasema hayo tukirejea kinachoendelea wakati huu ambao takribani wanafunzi 539,243 wanafanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne kote nchini.

Mtihani huo wa upimaji, unafanyika pamoja na ule wa maarifa (QT) ambao watahiniwa wake waliosajiliwa ni 9,865

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, anaonya na kusema, haiwezekani udanganyifu utokee katika shule ukafanikiwa bila ushiriki wa mkuu wa shule, mmiliki au mratibu wa elimu kata.

Siyo mara ya kwanza NECTA kutoa onyo kuhusu udanganyifu, kwani inaonekana umekuwa sugu, hivyo ingefaa wenye dhamana ya usimamizi wa mitihani kuzingatia utaratibu ili kusaidia taifa kupata viongozi wa baadaye.

Kwa ujumla, Tanzania inahitaji viongozi na wataalamu wa aina mbalimbali wa baadaye, katika sekta zote ikiwamo ya uchumi na huduma za kijamii wenye ufaulu usiopatikana kwa mazingira ya udanganyifu.

Hivyo, wakati huu ambao wanafunzi wa kidato cha nne wanaendelea na mitihani yao, ingekuwa ni vyema kama wataifanya kulingana na taratibu zinazotakiwa ili wafaulu kulingana na uwezo wao wa darasani.

Wanaofanya nitihani ni miongoni mwa wale wanaoandaliwa kuwa taifa la kesho, hivyo muda ambao baadhi yao wamekuwa wakiutumia kwa mipango ya udanganyifu wangeuelekeza katika kufanya vizuri mitihani hiyo.

Hatua hiyo inaweza kusaidia nchi kuwa na wasomi na wataalamu wenye uwezo mkubwa katika fani mbambali watakaochangia na kuharakisha maendeleo ya taifa lao kwa kutumia ujuzi walionao.

Lakini, njia hiyo ndiyo inayowezesha kuwapata wasomi wabobezi kuliko kuwapa wanafunzi ushindi feki ambao mbele ya safari katika masomo wanaweza kufanya vibaya kwa kukosa msingi mzuri wa elimu.

Kila heri wanafunzi wa kidato cha nne walioanza mtihani wiki hii, wafanye kwa kutegemea uwezo wao na jinsi walivyofundishwa na siyo njia ya mkato ambayo inaweza kuwafanya wasifae kuwa taifa la kesho.

# Wadau wa habari waipa mapendekezo serikali

**Na Mwandishi wetu**

WADAU wa Habari wamewasilisha serikalini mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazogusa sekta ya habari nchini.

Mapendekezo hayo yanagusa sheria na/au baadhi ya vifungu vya sheria ambavyo kwa mtazamo wa wadau wa habari nchini, vinakwaza kwa namna moja au nyingine uandishi wa habari na vyombo vya habari katika utekelezaji wa majukumu yake.

Akiwasilisha mapendekezo hayo kwa niaba ya wadau wengine jana mjini Dodoma kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri wa Habari Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema yalitokana na maoni ya wadau wote wa sekta ya habari.

Wadau hao ni kupitia Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CORI) (ambao TEF ni mwanachama wake, ukiunganisha taasisi 11 chini ya Uenyekiti wa Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Ni pamoja na TEF, Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika - Tawi la Tanzania (MISA - TAN), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (CIB), Twaweza, SIKIKA na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Balile alisema muhtasari uliowasilishwa unalenga kuiwezesha serikali kuzingatia mapendekezo ya wadau wa habari katika mchakato wa marekebisho ya sheria husika, kabla ya kupelekwa bungeni kwa ajili ya kupata baraka za Bunge.

"Sheria zilizochambuliwa katika muunganisho huu ni Sheria ya Huduma za Habari, 2016, Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, 2016 na ile ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta; (Maudhui ya Mtandaoni) Kanuni, 2020 na Sheria ya Uhalifu wa Mtandao, 2015,"alisema Balile.

Alitaja baadhi ya mambo ambayo wadau wanaomba kufanyiwa marekebisho au kubadilishwa katika Sheria hizo ni mamlaka ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) ambayo inaweza kufungia vyombo vya habari vinapodhaniwa au kutuhumiwa kuwa vimekosea, bila suala au makosa husika kufikishwa katika vyombo vya kisheria vya kiuamuzi kama Mahakama.

Jingine ni Sheria ya Huduma za Habari (MSA) kuanzisha vyombo vinne vya kusimamia sekta ya habari, tofauti na sekta au taaluma nyingine ambako masuala husika husimamiwa na chombo au mamlaka moja.

"MSA inaanzisha Bodi ya Ithibati, Mfuko wa kusomesha waandishi wa habari na Baraza Huru la Habari, sisi katika hili tunapendekeza kuwapo kwa chombo kimoja pekee cha kuratibu sekta badala ya kuwa na vyombo vingi," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea muhtasari wa mapendekezo hayo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Kijaji, alisema serikali itayafanyia kazi mapendekezo hayo kwa lengo la kuiwezesha sekta ya habari kuwa rafiki kwa wadau wake, hususan waandishi wa habari.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba sekta ya habari inakuwa rafiki na ni dhamira yetu sote kupiga hatua na kufikia malengo ya ufanisi utakaokuwa na faida kwa kila mmoja. Hatua ya leo ni mwanzo mzuri na ninaamini tutapiga hatua kwa faida ya taifa letu,"amesema.

Baada ya kupokea mapendekezo hayo, waziri huyo ameyakabidhi kwa Katibu Mkuu wake, Dk. Zainab Chaula pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Dk. Jim Yonazi kwa ajili ya kuanza kuyafanyiwa kazi.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya sekta ya habari, mawasiliano na teknolijia ya habari, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## NEC yapitisha 11 ubunge Ngorongoro

**Na Thobias Mwanakatwe,**

NGORONGORO

WAGOMBEA 11 kutoka vyama mbalimbali kati ya 14 waliochukua fomu ya kuomba kuteuliwa kuwania ubunge katika uchaguzi mdogo Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha, wameteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwania nafasi hiyo.

Msimamizi Mkuu wa uchaguzi huo ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ngorongoro, Dk. Juma Mhina, akizungumza na gazeti hili jana, alisema wagombea wa vyama vya CCK, AAFP na TLP hawakuteuliwa kutokana na kushindwa kurejesha fomu.

Dk. Mhina aliwataja wagombea na vyama vyao waliotcuteuliwa baada ya kutimiza masharti yote ya uchaguzi kuwa ni Emmanuel Lekishoni Shanghai kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Simon Jonhson Bayo (SAU), Amina Amiri Mcheka (NLD), Mary Moses Daudi (UPDP) na Frida Marko Nnko (UMD).

Wengine ni Paulo Mwita Makuru (UDP), Shafii Kitundu (ADC), Feruziy Feruziyson (NRA), Simon Ngilisho (Demokrasia Makini), Jonson Gagu (ACT-Wazalendo na Zuberi Hamis (ADA-TADEA). Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC, kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zilipaswa kuanza jana na zitahitimishwa Desemba 10 na siku ya kupiga kura itakuwa Desemba 11, mwaka huu.

Uchaguzi huo unafanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia CCM, William Tate Ole Nasha aliyefariki Septemba 27, mwaka huu.

# Taarifa Makonda kuvamia Clouds kuanikwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema ripoti ya kamati ya uchunguzi wa tukio la uvamizi wa kituo cha Redio cha Clouds FM, lililofanywa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Saalam, Paul Makonda, itatolewa baada ya kukamilika na kila mtu atafahamu nini ambacho kamati hiyo imebaini.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa yake kwa waandishi wa habari kuhusu mafanikio katika sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Dk. Kijaji akijibu swali lililohoji kuwa ni lini wizara hiyo haijatoa majibu ya kamati iliyoundwa na aliyekuwa wizara hiyo, Nape Nnauye, kuchunguza tukio la kuvamiwa kwa kituo hicho, alisema ripoti ya tukio hilo itakapokamilika itawekwa wazi.

Akizungumzia utekelezaji wa sheria ya habari kuhusu kanuni inayowataka waandishi wa habari kuwa na kiwango cha elimu ya Diploma ifikapo Januari 2022, alisema suala hilo linafanyiwa kazi kati ya serikali na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

"Kilitolewa kipindi cha waandishi wa habari kwenda kusoma ili kufikia katika kiwango cha Diploma, lakini hamjaenda kusoma kwanini? Lakini kwa kushirikiana na Jukwaa la Wahariri tayari wameshatuandikia ripoti yao ambayo sisi kama serikali tutakwenda kufanyia kazi na kutoa majibu kabla ya Januari 1, 2022," alisema Kijaji.

Kuhusu vyombo vya habari vilivyofungiwa na serikali, alisema wizara yake inaendelea kufanyia kazi maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa maslahi mapana ya pande zote.

"Jambo hilo lipo mezani kwangu na wizara tunaendelea na majadiliano kwa maslahi mapana ya pande zote na maamuzi yatatolewa," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Judith Nguli (kulia), akikabidhi taarifa ya vijiji vya Makata na Mitawa A kwa Meneja wa VETA, Kanda ya Kusini-Mashariki, Neema Mwakaluk-wa, kwa ajili ya utoaji wa ardhi ekari 50 ili kujenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha wilaya hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni ndogo kibiashara kuwezeshwa

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), inatarajia kutoa mafunzo kwa kampuni ndogo za kibiashara, kuboresha biashara, kujitangaza pamoja na kufungua fursa za kiuchumi kwenye soko la dunia.

Mafunzo hayo ambayo yanafanyika chini ya mradi wa Africa Franchising Accelerator Project (AFRAP), utakapokamilika utawanufaisha Watanzania na kutoa ajira zipatazo 80,000 utafanyika kwa miezi 48 ukitarajia kukamilika Januari, 2025.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Francis Nanai, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, alisema mradi huo ni fursa kwa wafanyabiashara hao, na kwamba taasisi hiyo iliingia makubaliano ya Sh. bilioni 2.2 na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), kutekeleza mpango huo.

"Juni 2016, Benki ya AfDB kwa niaba ya Sekta Binafsi Afrika (FAPA) tulisaini mkataba na TPSF kutekeleza mpango wa kuziinua kampuni za kiafrika na kujitangaza kwa makubaliano ya Dola 799,800 kutoka nchi za Japan na Austria.

"Mpango huu utapunguza kiwango cha uhaba wa ajira na kuchangia pato la taifa. AFRAP umelenga kutoa mbinu za kujikuza kwa watu 2,250 na kuongeza ajira za moja kwa moja 38,250 na zisizo za moja kwa moja 56,250 kwa Watanzania," alisema Nanai.

Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, alisema wanawake ni kati ya watakaonufaika na AFRAP kwa asilimia 50, kutokana na wanachama wa chama hicho, kuwa na vigezo kwa kiwango kikubwa kujiunga na mradi.

"Wanawake wa TWCC ni kati ya watakaonufaika na AFRAP kwa sababu asilimia 50 ya wanachama, biashara zao zinafahamika, zimesajiliwa, wanalipia kodi," alisema Mwajuma.

Kiongozi wa mradi huo, Wambugu Gichohi, alisema mafunzo ya siku sita yataanzia visiwani Zanzibar kisha mkoani Mbeya, Mwanza, Dodoma, Arusha na Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mchakato wa kuzipata kampuni zitazowezeshwa kukuza biashara zao.

"Vigezo vitazingatiwa, kampuni iwe na mauzo ya faida ya Sh. milioni 250 kwa mwaka, biashara iliyofanyiwa hesabu kwa miaka mitatu nyuma, iliyosajiliwa na mwendesha biashara awe halisi sio bosi wa kampuni au kiongozi fulani."

# Shaka aagiza uchunguzi utoaji zabuni

**Na Beatrice Shayo,** GEITA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ameagiza kufanyika kwa uchunguzi wa utoaji wa kazi kwa makandarasi Halmashauri ya Wilaya Geita, kwa kuwa kunaonyesha viashiria vya rushwa.

Alitoa maagizo hayo jana katika Kata ya Mgusu akiwa kwenye ziara ya wajumbe wa Sekretarieti ya CCM kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, kufanya uchunguzi wa suala hilo kujua kwanini Mhandisi ameamua kuondoka na mwingine kuondolewa na kukwamisha kazi, inaonyesha kuna tatizo.

"Ipo harufu ya rushwa hapa, fanyeni uchunguzi kubaini ni nini kinasababisha makandarasi hawa kujitoa. Tusije tukawalaumu kumbe tatizo lipo kwetu," alisema Shaka.

Aidha, Shaka alisema amepewa taarifa halmashauri hiyo kwa mwaka inakusanya zaidi ya Sh. bilioni 10, lakini fedha hizo hazilingani na miundombinu na huduma za maendeleo zinazotekelezwa.

Alisema wananchi wanalalamika ingawa kuna taarakimu nzuri za makusanyo, lakini uzuri wake hauonekani katika uboreshaji wa mji huo na huduma za kijamii.

"Wananchi wanalalamika kutokuwapo kwa miundombinu na huduma bora mfano; barabara nyingi hazina taa, zahanati vijiji vingi zimekamilika muda mrefu lakini hazijaanza kutoa huduma, masoko ya wafanyabiashara wadogo kukosa mazingira rafiki ya kufanyia biashara kwa kisingizio cha ufinyu wa bajeti. Hii haiko sawa,"alisema.

Alisema viongozi wa halmashauri hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji, Zahara Michuzi, kuhakikisha makusanyo ya mapato yanaendana na miradi ya maendeleo.

Shaka alitaka kuwapo uwazi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuitenganisha inayogharimiwa na mapato ya ndani, ruzuku ya serikali kuu na CSR, ili kuleta tija kwa wananchi na kuhakikisha fedha zinazopatikana zinatumika kwa ufanisi.

Aliagiza wachimbaji wadogo zaidi ya 2,000 katika Kata ya Mgusu wasikilizwe ombi lao la kuongezewa eneo la kutoka msitu wa Geita ili wafanye shughuli zao kwa amani na utulivu.


COLLEGES & INSTITUTES CANADA | COLLÈGES & INSTITUTS CANADA

collegesinstitutes.ca | collegesinstituts.ca

## MONITORING, EVALUATION AND LEARNING (MEL) OFFICER

Colleges and Institutes Canada (CICan) invites eligible candidates to indicate their interest in employment as a **Monitoring, Evaluation and Learning (MEL) Officer** to the Empowerment through Skills Program (ESP) in Tanzania, implemented by CICan in close collaboration with the Ministry of Education, Science and Technology (MOEST) through the Department of Technical and Vocational Training (DVET).

The **Monitoring, Evaluation, and learning (MEL) Officer** will act as the principal resource on all monitoring, evaluation and learning issues, practices, and tools relevant to the implementation of the project. The MEL Officer is primarily responsible for developing and implementing

**Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:**

i Full fluency in English and Swahili.
ii Tanzanian citizen or legally permitted to work in Tanzania. Note: CICan will not provide a work permit or sponsor individuals.
iii Master's degree or higher in one or more of MEL, statistics, economics, international development, or a related field.
iv At least 5 years of professional experience working on MEL on international development projects, ideally in the education or TVET sector.
v Strong analytical skills with the ability to collect, organize, analyze, and disseminate significant amounts of information.
vi Experience working with different types of data and different types of surveys.
vii Experience conducting research and synthesizing primary and secondary data.
viii Experience with impact evaluation and related methodologies (e.g., propensity score matching)
ix Proficiency with current statistical analysis and data visualization software (e.g., Power BI, SPSS, SAS, R, etc.).
x Experience using statistical techniques and software to determine correlations and attribution relationships (i.e., logit models).
xi Strong experience in mobile/ digital data technology (ODK/ONA preferred) including the ability to quickly digitalize/script large and complex surveys in XLS forms.
xii Understanding of content analysis of qualitative data; ideally with experience using qualitative data analysis techniques.
xiii Familiar with the design and implementation of results-based management and outcome mapping frameworks (e.g., Global Affairs Canada Logic Model and Performance Monitoring Frameworks).
xiv Experience developing data analysis plans and supporting data analysis teams.
xv Demonstrated ability to write up statistical analysis, study findings and other types of results in clear, concise, and error-free English.
xvi Experience working with an international team, government ministries at national and county level.
xvii Demonstrated competence in the planning, implementation, administration, and reporting of donor-funded projects, ideally with experience with Global Affairs Canada.
xviii Excellent organizational, communication, and interpersonal skills.
xix Ability to work both independently and collaboratively on a team.
xx Very strong writing, computer, and data skills.

Interested candidates should send their applications electronically ONLY to **info@tz.collegesinstitutes.ca** no later than **28th November 2021**. Only shortlisted candidates will receive a detailed job description.

**The application should comprise of:**

- Curriculum Vitae (CV)
- Cover Letter.
- Copies of relevant certificates, permission to work in Tanzania; and
- Name, physical addresses, and contact details of three references who can comment on personal conduct and previous work done.

216574301



COLLEGES & INSTITUTES CANADA | COLLÈGES & INSTITUTS CANADA

collegesinstitutes.ca | collegesinstituts.ca

## GENDER SPECIALIST COLLEGES AND INSTITUTES CANADA, DAR ES SALAAM

Colleges and Institutes Canada (CICan) invites eligible candidates to indicate their interest in employment as **Gender Specialist** to the **Empowerment through Skills Program (ESP)** in Tanzania, implemented by CICan in close collaboration with the Ministry of Education, Science and Technology (MOEST) through the Department of Technical and Vocational Training (DVET).

The **Gender Specialist** will be responsible for supporting general program activities and to specifically provide effective and efficient gender equality (GE) activities support to the ESP project office in Tanzania. Duties will include but not be limited to supporting the Senior Technical Advisor (Gender), implementing recommendations from the gender analysis, implementing gender equality strategies, and supporting project partners and stakeholders.

**Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:**

i Fluency in English and Swahili.
ii Tanzanian citizen or legally permitted to work in Tanzania. Note: CICan will not provide a work permit or sponsor individuals.
iii Bachelor's degree or equivalent in gender studies, development, or a related field.
iv A minimum of 5 years' professional experience in a similar role with an international organization working on gender on international development projects, ideally in the education or TVET sector.
v Superior written and verbal English and Swahili communication skills along with the ability to effectively present and clarify requirements, expectations, ideas, and concepts to various audiences/stakeholders
vi A minimum of 5 years' proven experience combining formal expertise on gender mainstreaming and gender equality with experience of applying these concretely to specific development sectors, plans, policies, and business processes.
vii Strong analytical skills with the ability to collect, organize, analyze, and disseminate significant amounts of information.
viii Familiar with development cooperation and working with international organizations.
ix Demonstrable Monitoring, Evaluation and Learning experience of social projects
x Demonstrated competence in the planning, implementation, administration, and reporting of donor-funded projects, ideally with experience with Global Affairs Canada or a similar organization.
xi Excellent organizational, communication, and interpersonal skills and Strong writing, computer, and data skills.
xii Ability to work both independently and collaboratively on a team.

Interested candidates should send their applications electronically ONLY to **info@tz.collegesinstitutes.ca** no later than **28th November 2021**. Only shortlisted candidates will receive a detailed job description.

**The application should comprise of:**

- Curriculum Vitae (CV)
- Cover Letter.
- Copies of relevant certificates, permission to work in Tanzania; and
- Name, physical addresses, and contact details of three references who can comment on personal conduct and previous work done.

216574301

# Mwandishi nguli: Mchango wa wawekezaji wazawa uthaminiwe

**Na Elizabeth Zaya**

MWANDISHI nguli na aliyewahi kuwa mwandishi wa habari wa Mawaziri Wakuu wastaafu, Edward Lowassa na Mizengo Pinda, Said Nguba, amesema kuna haja ya kuwathamini na kutambua mchango wa wawekezaji wazawa katika kuinua uchumi wa nchi.

Nguba alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam aliposhiriki hafla ya uzinduzi rasmi wa nyumba za makazi, uwekezaji uliofanywa na mzawa, Said Msonda katika eneo la Boko Basihaya, Kinondoni Dar es Salaam.

Alisema Watanzania wamejenga utamaduni kwamba watu wenye uwezo wa kuwekeza ni wa kutoka nje ya Tanzania pekee, jambo ambalo siyo kweli.

"Inabidi ifike mahali na sisi Watanzania tujione na kujiamini kwamba tunaweza kufanya mambo makubwa, hii tabia ya kusema kwamba wazawa hawana uwezo wa kuwekeza inabidi ife, tumekusanyika kwa wingi wetu hapa kushuhudia uwekezaji mkubwa wa majumba haya makubwa ambayo wanayaita 'Appartments' ambayo yamewekezwa na Mtanzania mwenzetu huyu Msonda,"alisema Nguba.

"Hivi kwani huyu ametoka nje ya Tanzania? Ifike wakati tubadilike na tujiamini na tuwathamini na kutambua mchango wa wawekezaji wetu wa ndani. Hii kazi aliyofanya hapa si ndogo, amejenga nyumba hizi na zinasaidia kutoa huduma kwa wananchi, na kupitia hizi anatoa ajira na kulipa kodi, hivyo kukuza uchumi wetu, haya ndio viongozi wetu wakuu wanatusisitiza kila siku tuyafanye."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Basihaya, Andrew Samson, alisema wawekezaji kama Msonda wanatakiwa watumiwe na wananchi kujifunza namna ya kufanikiwa na kujenga jamii yenye maendeleo.

"Binafsi nimejifunza jambo kubwa kupitia tukio hili la leo, na nimeamini kila kitu kinawezekana tukijenga jamii ya kujiamini na kufanya kazi kwa bidii. Msonda angeweza kwenda kuwekeza hata nje ya Tanzania kwa hatua aliyofikia, lakini ameona afanye hapa nchini na kuinufaisha nchi na watu wake, watu kama hawa waungwe mkono," alisema Andrew. Kwa upande wake, Msonda alisema siri iliyochangia yeye kufikia katika hatua hiyo aliyonayo kwa sasa ni kufanya kazi kwa bidii, kuwa na nidhamu ya kujinyima baadhi ya mambo ambayo siyo ya muhimu sana na kutunza akiba kidogo kidogo.

"Kwa kweli niseme tu kwamba mimi nimetoka katika mazingira ya kawaida sana, na nimefanya kazi za kuajiriwa kwa kipindi kirefu sana, katika miaka yote kazini, kila nilichokuwa nakipata nilikuwa najitahidi kujiwekea akiba na sikuwa ni mtu wa starehe sana hata marafiki zangu walikuwa wananishangaa, kwa hiyo kila nilichokuwa nikikipata nakiweka kwenye maendeleo hadi hapa nilipofikia leo nashukuru Mungu," alisema Msonda.

Miongoni mwa huduma ambazo zimewekwa katika makazi hayo ni saluni kwa ajili ya kunyoosha viungo vyenye shida hususani wanaopatwa na magonjwa ya kiharusi na huduma nyinginezo pamoja na maduka makubwa.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Saumu Kumbisaga (katikati), akizungumza na wafanyakazi wa kampuni ya madini ya OreCorp Tanzania Ltd, wakati wa kampeni ya ufahamu na umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19 katika viwanja vya eneo la mradi wa mgodi wa Nyanzaga, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kampuni yawapa wafanyakazi wake elimu ya corona

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya OreCorp Tanzania Ltd (OreCorp) imeunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza katika kampeni ya kutoa elimu ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Kampeni hiyo inalenga katika kujenga ufahamu ili kupambana na maambukizi ya UVIKO -19 katika wilaya hiyo.

Hatua hiyo inafuatia matembezi katika mgodi wa dhahabu wa Nyanzaga yaliyofanywa Jumapili na kuongozwa na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Dk. Saumu Kambisaga na timu yake kwa lengo la kutoa mafunzo, elimu pamoja na chanjo kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo.

Akizungumzia zoezi hilo, ikiwa ni awamu ya matembezi hayo katika mgodi huo ndani ya miezi kadhaa, Dk. Kambisaga aliishukuru OreCorp kwa kuendelea kutuunga mkono kwa kutoa elimu na ufahamu kuhusu janga hili. Pia aliwashauri wananchi kwenda kupata chanjo kwenye vituo vya huduma.

Aidha, OreCorp imeendelea kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake, washauri na wageni wanaotembelea mgodi wa mradi wa Nyanzaga wanachukua tahadhari za kutosha kuhusiana na UVIKO-19 ikiwamo kupima viwango vya mwili joto, kuosha mikono kwenye vituo maalum.

Meneja Mkuu wa OreCorp, Damien Valente, alisema kuwa kampuni hiyo inachukua hatua kuhakikisha kuwa usalama wa wafanyakazi wake ni kipaumbele kwenye mgodi huo.

"Kama kampuni tunaendelea kutoa mafunzo kwa kila anaehusika kwenye mradi huu ili waweze kujilinda wenyewe pamoja na watu wanaowazunguka dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19," alisema na kuongeza:

"Pia tunafurahi kuwa tumeweza kuiunga mkono Wilaya ya Sengerema kupitia Afisa Afya wa wilaya katika kuongeza ufahamu juu ya manufaa ya kupata chanjo na kutimiza sehemu ya wajibu wetu dhidi ya janga hili."

# Wananchi watoa ardhi kujenga chuo cha VETA

**Sabato Kasika**

WAKAZI wa vijiji vya Makata na Mitawa A, wilayani Liwale, Mkoa wa Lindi, wametoa ekari 50 za ardhi ili kujenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), kusaidia vijana kupata ufundi wa fani mbalimbali utakaowawezesha kujiajiri.

Akipokea taarifa ya makubaliano ya wakazi hao kutoka kwa Mkuu wa wilaya hiyo, Judith Nguli jana, Meneja wa VETA Kanda ya Kusini-Mashariki, Neema Mwakalukwa, aliwapongeza wananchi hao kwa uamuzi huo.

Meneja huyo alisema utoaji wa ekari hizo umeongeza uzito ambao unaonyesha kuwa wananchi hao wanahitaji chuo hicho ambacho kitakuwa na manufaa kwa wilaya hiyo na maeneo mengine.

"Chuo kikishajengwa na kukamilika kitasaidia watu mbalimbali wakiwamo vijana na watu wazima kupata elimu ya ujuzi wanaotaka, hasa kwa kuzingatia kwamba mafunzo ya VETA hayachagui umri," alisema Neema.

Neema alisema taarifa hiyo ataifikisha kwa wakubwa wake, ili kuweka mikakati ya ujenzi huo ikiwamo kutathmini gharama za ujenzi, kisha mikakati yote ya kufanikisha ujenzi huo itatolewa.

Mkuu wa wilaya hiyo, Judith Nguli, alimshukuru meneja huyo kuitikia ombi la wana Liwale la kuhitaji chuo VETA, na kwamba kitendo chake cha kufika kuchukua taarifa ya makubaliano yao ya kutoa ardhi imeonyesha anajali.

"Lakini pia hatua ya wakazi wa vijiji vya Makata na Mitawa A kutoa ardhi yao inaonyesha ni jinsi wanavyounga mkono mkakati wa serikali wa kutaka kujenga chuo cha VETA kila wilaya," alisema Judith. Alisema, kwa sasa serikali inaendelea na mkakati wa kujenga vyuo vya VETA katika kila wilaya na kwamba, kitendo cha wakazi wa vijiji hivyo kutoa ardhi, ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuwa na VETA kila wilaya.

Mtendaji wa Kata ya Makata, Hadija Eriyo, alisema iwapo chuo hicho kitajengwa na kukamilika, kata hiyo itachangamka, kwa kuwa itapokea watu mchanganyiko na pia shughuli za kiuchumi zitaongezeka.

"Wito wangu ni kwamba, wananchi wote wa Liwale wawe tayari kushiriki kwa hali na mali katika ujenzi wa chuo, kwani hakitakuwa kwa ajili ya wakazi wa Kata ya Makata, bali Liwale nzima," alisema Hadija.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mitawa 'A', Ahmad Mchijila, alisema, wamekubaliana na wenzao wa Makata kutoa ardhi hiyo bila masharti ili kusaidia vijana wa vijiji hivyo na wilaya kwa ujumla kupata elimu ya ufundi.

"Awali eneo tulilolota lilikuwa ni shamba la ushirika ambalo wakazi wa vijiji vyote tulikuwa tunalima mazao mbalimbali, lakini sasa tumekubaliana kubadili matumizi ili kujenga chuo cha VETA," alisema Mchijila.

Katika kubadili matumizi ya ekari hizo, walianza kujenga majengo mawili, kwa ajili ya sekondari. Lakini wakaachana na mpango huo kwa kuwa tayari sekondari nyingine ipo na sasa wanataka chuo cha VETA.

## HABARI KITAIFA

# Usalama, afya za wafanyakazi vituo vya mafuta kuboreshwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na Chama cha Wamiliki na Waendeshaji wa Vituo vya Mafuta Nchini (TAPSOA), wamekubaliana kushirikiana katika kuboresha hali ya usalama na afya za wafanyakazi wa vituo vya mafuta.

Ushirikiano huo ni kupitia ukaguzi, mafunzo pamoja na ushauri utakaokuwa unatolewa na wataalam wa OSHA katika vituo hivyo.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika kikao cha mashauriano baina ya menejimenti ya OSHA na wanachama wa TAPSOA wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kilichofanyika jijini Mwanza ambapo pande hizo mbili zilikutana kujadiliana kuhusu namna bora ya kutekeleza Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake.

Kikao hicho kilifunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ambaye pamoja na kusisitiza OSHA na TAPSOA kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa sheria tajwa, alielezea umuhimu wa sekta ya mafuta katika uchumi wa nchi.

"Nani anasema nyinyi hamjachangia nchi hii kufikia uchumi wa kati, kimsingi mmekuwa na mchango mkubwa katika kufika uchumi wa kati. Kama nchi tunataka kupambana na umaskini na nyinyi ni wadau muhimu ambao mtatusaidia katika hilo kama nilivyoelezwa awali hapa kwamba asilimia 66 ya wawakezaji wa vituo vya mafuta nchini ni Watanzania na zaidi ya asilimia 60 ya wafanyakazi katika sekta hii ni wanawake hivyo mnaweza kuona jinsi sekta hii ilivyo muhimu katika uchumi na maendeleo ya Taifa letu na kwasababu hiyo ni lazima tuitunze ili nayo itutunze," alisema Mhagama.

Katibu Mkuu wa TAPSOA, Augustino Mmasi, ambaye alikuwa mwenyekiti mwenza wa kikao hicho, alisema wanachama wake wanaamini kwamba endapo hoja na mapendekezo yao yanayotolewa kupitia vikao mbalimbali vya kuelimishana, basi azma ya serikali ya kuondoa ama kudhibiti vihatarishi katika sehemu za kazi itaweza kufikiwa.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema chimbuko la makubaliano hayo ni tathmini iliyofanywa na Taasisi yake katika usimamizi wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ambayo ilibainisha ombwe katika ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za usalama na afya nchini ambazo ni muhimu katika uundaji wa sera za nchi zinazohusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

"Tulifanya tathmini ya namna tunavyosimamia masuala ya usalama na afya nchini na kubaini kwamba kwa utaratibu tuliokuwa nao ilikuwa ni vigumu kuyafikia maeneo mengi ya kazi, kufanya ukaguzi na kushauri namna ya kuboresha zaidi mifumo ya usalama na afya hivyo tukaja na utaratibu wa kufanya kaguzi zetu kisekta ambapo kupitia utaratibu huto tumepata mafanikio makubwa ikiwamo kuzifikia sekta zote muhimu ikiwemo sekta ya madini, mawasiliano, huduma za fedha, bandari na viwanda," alisema Mwenda




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) PLC, Michal Bachan, akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea kiwanda cha TCC, Barabara ya Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Kulia ni Mkurugenzi wa Mahusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Patricia Mhondo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mkumbo aeleza umuhimu wa bidhaa bora

**Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeitaka Wizara ya Viwanda na Biashara na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuchukulia kwa uzito mkubwa ushiriki wa shindano la tuzo ya bidhaa bora yanayoandaliwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Agizo hilo lilitolewa jijini Dar es Salaam jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, wakati wa uzinduzi wa Tuzo ya Ubora wa Bidhaa Kitaifa kwa mwaka 2021, JIJINI Dar es Salaam.

Alisema wao kama wizara tuzo hizo wanazichukulia kwa uzito mkubwa kwa sababu ni maandalizi muhimu sana ya kuingia kwenye soko kubwa la biashara la Afrika.

Alisema tuzo hizo ni muhimu kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia kuingia kwenye Soko Uhuru la Biashara Afrika lenye uchumi wa wastani wa Sh. bilioni 3.2. Alisema huo ni uchumi mkubwa, hivyo Tanzania inaenda kushiriki tuzo hizo kwa lengo la kushindana.

"Kwa hiyo ni lazima sasa bidhaa zetu zikae kikanda kikanda na kimataifa.

Kuziduliwa kwa tuzo hizi za kitaifa za bidhaa bora zinatusogeza huko, kwani ubora ni sehemu ya mipango ya Serikali ya kuendelea kuboresha huduma kwa ubora wa bidhaa," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema bidhaa kukidhi viwango vya kikanda na kimataifa ni jambo la msingi sana na haya ni maandalizi ya ushiriki kwenye mashindano ya tuzo za ubora za SADC.

Kwa mujibu wa Prof. Mkumbo, Tanzania ilikuwa hajawahi kushiriki tuzo za SADC, kwa hiyo ni lazima kuandaa wafanyabiashara nchi ili waweze kushiriki kwenye kunyang'anyiro cha tuzo hizo.

"Kwenye upande wa SADC wenzetu walishaanza siku nyingi, mara ya kwanza shindano hilo lilifanyika mwaka 2011 kwa hiyo 2019 yalikuwa mashindano ya tisa na mwaka jana (2020) hayakufanyika (kutokana na changamoto ya UVIKO 19) kwa hiyo mwaka huu yatakuwa ni mashindano 10, hivyo hii ni hatua muhimu ambayo tunachukua na ni lazima tutashinda."

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alisema tuzo za ubora kitaifa zinazolenga kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa na huduma katika Ukanda wa SADC. Alisema jukumu la kuandaa tuzo hizo limekabidhiwa kwa shirika hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

"Tumekabidhiwa jukumu la kuanzisha Tuzo za Ubora za kitaifa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufuatia makubaliano baina ya wanachama wa SADC ili kutambua na kukuza sekta ya biashara kupitia ubora wa bidhaa na huduma katika ukanda huu,"alisema.

## Mkazi Dar azoa bajaji ya Bonge la Mpango

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa Droo ya Nne ya Msimu wa Pili wa Kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB 'NMB Bonge la Mpango - 2merudi Tena,' Richard Jeremiah Iranga, amekabidhiwa pikipiki ya miguu mitatu aina ya Skymark yenye thamani ya Sh. milioni 4.5.

Iranga, ambaye ni mfanyabiashara wa mazao na mkazi wa Goba, wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, alikabidhiwa pikipiki hiyo jana na Meneja wa NMB Tawi la Mlimani City, Deogratius Kawonga, hafla ya makabidhiano ikifanyika Viwanja vya Stendi ya Daladala ya Mawasiliano 'Simu 2000.'

Akizungumza kabla ya kukabidhi zawadi hiyo, Kawonga alisema NMB Bonge la Mpango ni kampeni ya miezi mitatu, inayohamasisha utamaduni chanya wa kuweka akiba, ambako kila wiki washindi 10 huzawadiwa pesa taslimu Sh. 100,000 kila mmoja, huku wengine wawili wakitwaa pikipiki ya Skymark ya Sh. milioni 4.5 (moja kwa kila mshindi.

Wiki 12 za droo hiyo, zitazalisha jumla ya washindi 170 watakaozoa zawadi zenye thamani ya Sh. milioni 237, kigezo cha ushiriki kikiwa ni kufungua akaunti na kuweka angalau Sh. 100,000 ama mteja mwenye akaunti kuweka akiba isiyopungua kiasi hicho.

Kwa upande wake, Iranga alieleza kufurahia zawadi hiyo, na kwamba kwake ni zaidi ya mtaji, kwani itaenda kumpunguzia gharama za usafirishaji wa mazao ya biashara kutoka sehemu moja kwenda nyingine, ambao ulikuwa unamgharimu pesa nyingi na kumpa wakati mgumu.

## Sungusungu 300 kukabili wahalifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa vijiji sita vya Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameanzisha jeshi la jadi (Sungusungu) lenye askari 300 na kupatiwa mafunzo maalum kwa ajili ya kukabiliana na vitendo vya uhalifu, uporaji wa mifugo na madini katika maeneo yao.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, John Mahona, aliyabainisha hayo juzi katika hafla ya kuwasimika walinzi hao wa jadi kutoka vijiji sita vya kata hiyo ambapo hatua hiyo inakuja baada ya kushamiri kwa matukio mbalimbali ya uhalifu vijijini.

Aidha alisema, kata hiyo inamwingiliano mkubwa wa watu kutoka sehemu mbalimbali kwa sababu ya uwapo wa shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu katika mgodi mdogo wa Wisolele sanjali na uwapo karibu wa makao makuu ya halmashauri hiyo, hivyo baadhi ya vijana wamekuwa wakifanya uhalifu.

"Vijana hawa 300 wamepewa mafunzo maalumu kwa ajili kukabiliana na matukio ya watu kuvamiwa na kuporwa mali zao nyakati za usiku na baadhi watu wasiokuwa waadilifu na kwa uwapo wa jeshi hil tutakomesha vitendo hivyo," alisema Mahona.

Nae Mtemi mkuu wa Sungusungu wa kata hiyo, Wilson Kengele, alisema kabla ya kuwapo kwa walinzi hao wa jadi,matukio ya wizi wa ng'ombe na mbuzi, madini na uporaji wa maduka vijijini yalishamiri.

Ukurasa 14

Wapigakura wa Mlima Kenya wanavyopasua kichwa Ruto, Odinga

Ukurasa 12





# siasa

JUMATANO NOVEMBA 17, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

## SUDAN YAMKINI SI SHWARI TENA

BUNDI NDANI YA CUF

# Waliovuliwa wanapotinga Ofisi ya Msajili

## Wadau wakiona kiama cha chama hicho

**Na Sabato Kasika**

SINTOFAHAMU ya makada 10 wa Chama cha Wananchi CUF wanaodai kuvuliwa uanachama kitatanishi, umefikia hatua nyingine, baada ya kutinga rasmi Dodoma kwenye ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Wamefikisha malalamiko yao kwa msajili," anasema Sisthy Nyahoza, Naibu Msajili wa vyama, anapozungumza na Nipashe na kuongeza kuwa madai yao yalipokelewa jana na yatafanyiwa kazi na watapewa maelezo.

Anaendelea kusema: "Niko safarini, lakini nimeshapata taarifa kuwa wameyafikisha ofisini. Tutayapitia na watapewa majibu, hivyo uamuzi ambao utatolewa na ofisi ya msajili utaupata," anaahidi.

Anasema, ofisi hiyo ina jukumu la kulea vyama vya siasa ikiwamo kutatua migogoro inayovikabili, na kwamba ina wajibu wa kupokea malalamiko au kuingilia migogoro ili kudumisha ustawi wa demokrasia.

Ni mara ya pili bundi kuingia CUF, ya kwanza ilihusisha mgogoro wa kiuongozi baada ya uchaguzi mkuu wa 2015, uliosababisha wanachama kadhaa pamoja na Katibu Mkuu Seif Shariff Hamad, kujiunga na ACT-Wazalendo, na sasa kinajikuta tena kwenye mgogoro wa madai ya kuvuliwa uanachama kitatanisha.

Makada hao 10 waliotemwa uongozi na uanachama ni pamoja na Makamu Mwenyekiti wa CUF Zanzibar, Mussa Haji Komba, mgombea mwenza wa urais 2020, Hamida Abdallah Weshi wanaopinga kuenguliwa.

Sababu za kwenda kwa msajili huyo ni kutaka tafsiri ya uamuzi wa kikao kilichowavua uanachama mwanzoni mwa mwaka huu, wanachodai kina ukiukwaji wa taratibu za kisheria.

Abdul Kambaya ni miongoni mwa waliokumbwa na fagio hilo la CUF, ambaye anadai kuwa utaratibu uliotumika kuwavua uanachama haukufuata misingi ya katiba ya chama hicho ikiwamo kutotimia kwa akidi ya wajumbe.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Kambaya anadai, pamoja na akidi kutotimia, vilevile waliingizwa wajumbe feki kwenye kikao kilichowaondoa kwenye chama hicho.

**KUELEKEA KIAMA**

Katika mahojiano na Nipashe kuhusu mkwamo huo, baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa wanauchukulia mgogoro huo wa kisiasa kama kiama cha CUF.

Maggid Mjengwa ni mchambuzi wa siasa ambaye anasema, huenda huo ukawa ni mwisho wa umaarufu wa chama hicho katika siasa za Tanzania iwapo viongozi wake hawatachukua hatua za kusawazisha mambo.



Naibu Msajili wa Vyama vya siasa, Sisthy Nyahozza.

Anasema, kawaida tofauti zozote katika vyama humalizwa ndani ya vikao, na kwamba inapofikia wanachama wanatoka hadharani kueleza udhaifu wa viongozi wao, kuna jambo.

"Kwanza inawezekana hao wanaotoka nje kuzungumzia mambo ya vikao vya chama hawajui taratibu au wamejaribu kuzifuata imeshindikana na sasa wameona na liwalo na liwe," anasema Mjengwa.

Anasema, chama kinapofikia hatua hiyo, kuna uwezekano wa kukosa nguvu za ushawishi kwa wananchi, kwamba ni vyema viongozi wa chama hicho wakatafakari na kupata ufumbuzi.

Mchambuzi huyo anasema, viongozi wa CUF wangejifunza kupitia mgogoro wa kwanza kati ya Katibu Mkuu Hamad na Mwenyekiti Profesa Ibrahimu Lipumba, ambao umesababisha chama hicho kukosa nguvu, na kwamba wakiendelea kuulea anadai kitawafia mikononi.

"Ukiangalia CUF inadhoofika, haina nguvu kama zamani kutokana na mgogoro wa kwanza, sasa unaibuka mwingine, katika mazingira hayo hakiwezi kuwa imara," anaonya.

**CHANZO CHA MIGOGORO**

Abbas Mwalimu, mchambuzi wa siasa kutoka Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam, anaihusisha migogoro ndani ya vyama, katiba na falsafa.

Anasema, "Vyama vingi havina falsafa na badala yake vinapata wanachama kutokana na mtindo wa kufuata umaarufu wa mtu, na kwamba mtindo huo unasababisha viwe na migogoro."

Anataja katiba za vyama, ambazo wakati mwingine zina matatizo ambayo yanaweza kusababisha wanachama wahoji na wanapouliza unapoibuka migogoro hadi kuhama, ni eneo jingine.

Anasema, chama kuondokewa na wanachama ni hatari kwa ustawi na kwamba ni vyema vyama vikaanza kutafakari upya kuhusu falsafa na katiba kama zake iwapo zina upungufu.

"Kwa mfano upande wa katiba kwa muda mrefu wapo wenyeviti wa vyama ambao wameendelea kushika nafasi hizo muda mrefu na inawezekana hilo limesababisha wana CUF kuhoji, wakachukuliwa hatua," anasema.


Anasema, mgogoro wa CUF unaweza kuwa mpana zaidi, kwa madai kwamba Msajili anaangalia katiba ya chama hicho inasemaje, na kwamba uamuzi wake ndiyo wenye hatima ya wanachama hao.

"Uamuzi unaweza kuwarudisha au kuhamia chama kingine au waanzishe kipya, lakini wowote kati ya huo, unaweza ukaifanya CUF kuendelea na mgogoro," anasema.

**MSIMAMO WA CUF**

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho bara, Magdalena Sakaya, anapinga madai ya taratibu kukiukwa na kusisitiza kuwa zilifuatwa ikiwamo kuwa na wajumbe halali waliotakiwa na kutimiza akidi kama katiba inavyoelekeza.

"Kikao cha maadili siyo lazima kiwe na mwanasheria kina wajumbe watano wa lazima ambao ni Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar, Manaibu Katibu Mkuu Bara na Zanzibar na Mkurugenzi wa Itifaki na Mafunzo," anasema Sakaya na kuongeza kuwa wajumbe watatu wanaweza kuongezwa ikimpendeza mwenyekiti.



Watiania kwenye uchaguzi mkuu wa 2022, Raila Odinga (kushoto) na William Ruto, ndani ya harakati za kisiasa nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

# Wapigakura wa Mlima Kenya wanavyopasua kichwa Ruto, Odinga

**Na Mwandishi Wetu**

KENYA inaelekea kwenye uchaguzi mkuu Agosti mwakani kuchagua rais, wabunge, maseneta, magavana na wajumbe wa mabaraza ya kaunti.

Hata hivyo, kutokana na historia za kisiasa na kijamii, kuna ishara za hofu kujitokeza juu ya masuala kadhaa, ikiwamo idadi ndogo ya wanaojiandikisha kupiga kura.

Kufanyika kwa uchaguzi huo kunatarajiwa kuibua ushindani mkali kati ya upande unaomuunga mkono Makamu wa Rais, William Ruto na kinara wa upinzani anayeegemea upande wa Rais Uhuru Kenyatta, akitokea Chama cha Orange Democratic Movement (ODM), Raila Odinga.

Wanasiasa hao watatu wamekuwa na historia ya kushirikiana na wakati mwingine kuachana katika kipindi cha uchaguzi mkuu kwa miaka iliyopita.

Kubwa ni tukio la mwaka 2007, wakati matokeo ya uchaguzi mkuu yalipoibua vurugu, mapigano na mauaji.

Wakati huo, Ruto alikuwa anamuunga mkono Odinga lakini Kenyatta akiwa upande wa Rais mstaafu Mwai Kibaki.

Kutokana na vurugu na mauaji ya baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2007, Ruto na Kenyatta walikuwa miongoni mwa washtakiwa sita waliofunguliwa kesi kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) nchini Uholanzi.

Wakati mashtaka hayo yakiendelea Ruto na Kenyatta walishiriki uchaguzi mkuu wa 2013 Kenyatta akigombea urais na Ruto mgombea mwenza au makamu wa rais, baada ya ushindi.

Hivi sasa viongozi hao wawili wanajiandaa kuingia kwenye uchaguzi mkuu mwakani wakiwa 'hawapikiki chunga kimoja'. Japo si jambo geni katika mwenendo wa siasa na uchaguzi wa Kenya.

Wanasiasa Ruto na Odinga, wamejikita katika maeneo mengi ya nchi hiyo wakijinadi ili wachaguliwe, ingawa katika uhalisia wake, eneo wanaloliangazia zaidi ni ukanda wa Mlima Kenya.

Ruto amekuwa akijinasibu kwamba ngome yake ya kisiasa ipo mahali hapo, mtazamo ambao unapingwa na upande wapambe wa Odinga.

Miongoni mwa wanaochochea hisia za Ruto kukubalika huko ni hatua ya karibuni ya mwanasiasa aliye mbunge wa Gatundu Kusini, Moses Kuria, kutangaza kuihama Jubilee Februari mwakani.

Hatua hiyo ya Kuria inaweza kutafsiriwa kama ni moja vya viashiria vya kutanuka kwa kambi ya Ruto kuelekea uchaguzi mkuu huo.

Akihojiwa na televisheni ya Citizen nchini humo hivi karibuni, Kuria anasema, "hivi sasa nimefika ukomo dhidi ya Jubilee. Nitajiondoa mwaka ujao...nimejikita kuwasaidia watu washinde uchaguzi."

Hata hivyo, anasisitiza kuwa na matamanio ya kufanya kazi na Naibu wa Rais Ruto anayemtaja kuwa ni rafiki yake wa miaka mingi, ingawa mazingira yaliyopo hayamruhusu.

"William Ruto ni rafiki yangu, tumehangaika pamoja. Niling'olewa kutoka Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Usafiri kwa sababu ya mahusiano yangu na Ruto," anadai.

"Washirika wa Ruto 'wametazamwa' kuwa wapinzani ndani ya Jubilee kwa muda mrefu," anasema Kuria anayedai pia aliondolewa ujumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha kutokana na ushirika na Ruto.

Anaongeza kuwa kupunguza ushirikiano na Ruto kunafanyika ili kukinusuru kuanguka Chama chake cha Kazi (CCK).

Odinga anawategemea zaidi viongozi wa jamii zinazoishi kwenye ukanda wa Mlima Kenya wakiwamo magavana, wabunge, maseneta na wazee maarufu, ili kuungwa mkono.

Miongoni mwa magavana wanaotegemewa na Odinga Lee Kinyanjui wa Nakuru, Francis Kimemia wa Nyandarua, James Nyoro wa Kiambuu na Ndiritu Mureithi wa Laikipia.

Marafiki wa Rais Kenyatta katika ukanda wa Mlima Kenya anapotokea, wakiwamo Peter Kenneth, mbunge wa kuteuliwa, Maina Kamanda na Kanini Kega wa Kieni wanaowekwa kwenye orodha wa vinara wanaotegemewa na Odinga 'kunyakua' kura kwenye ukanda huo.

Ili kuwavutia watu wengi kushiriki mikutano yake, Odinga amekuwa akiwatumia wasanii kama Ben Githae, Sarafina Salim na Jose Gatutura.

Katika ziara kwenye kaunti zilizopo ukanda huo, Raila amefanikiwa kuongozana na magavana saba kati ya 10 waliopo huko, hivyo kutoa taswira ya namna anavyoungwa mkono.

Lakini, Mwakilishi wa Wanawake katika kaunti ya Nyandarua aliye mfuasi wa Ruto, Faith Gitau, hakualikwa kwenye ziara ya Odinga, akiamini kwamba ni sahihi kwa vile eneo hilo lipo huru kwa kila mwanasiasa kufika.

"Mimi pamoja na tunaomuunga mkono Ruto hatukualikwa, wakazi wa Nyandarua wana busara na wanamjua kiongozi watakayempigia kura 2022," anasema Faith.

Kama ilivyokuwa kwa Raila, Ruto naye, miongoni mwa maeneo mengine, alifika kaunti ya Kiambu akitafuta kuungwa mkono kutoka ukanda wa Mlima Kenya.

Kiambu ndipo nyumbani kwa Rais Kenyatta ambapo Ruto alihutubia mikutano kwenye maeneo ya Juja, Ruiru, Githunguri na mjini Kiambu na kufanya mikutano kama hiyo kwenye Jimbo la Gatanga huko Murang'a.

Hata hivyo, Ruto amekuwa akilichukulia eneo hilo kama sehemu yenye ngome yake kisiasa, lakini upande wa Odinga anapinga mtazamo huo.

Odinga amewahi kuzungumza aliposhiriki ibada kwenye kanisa la AIC huko Naivasha, kwamba ahitaji ruhusa yoyote kuingia kwenye maeneo ya ukanda wa Mlima Kenya.

Anayasema hayo alipomjibu Ruto ambaye siku chache kabla ya hapo, alitamka akiwa Laikipia, kwamba kiongozi huyo wa ODM ana hiari ya kulitembelea eneo hilo ingawa wakazi wake wameshafanya uamuzi wa nani watakayemchagua kuwa Rais.

"Nyahururu ni kituo cha kwanza katika kuupanda Mlima Kenya. Nimewasikia baadhi ya watu wakisema Odinga anapaswa kupata kibali chao kuingia kwenye eneo hilo," Raila anasema.

Odinga akatoa mfano uliomhusu baba yake mzazi, Hayati Jaramogi Oginga Odinga, kwamba aliingia mlimani hapo kwa mara ya kwanza na kuhakikisha Jomo Kenyatta anaachiwa huru kutoka jela na kuwa Rais wa kwanza wa taifa hilo.

Anaongeza, "nilishapanda mlima huu siku nyingi zilizopita nilipomuunga mkono Mwai Kibaki. Nilipokuja na kauli mbiu ya Kibaki Tosha, nilijua alikuwa Mkikuyu na Wakikuyu ni Wakenya."

Anasema wakati Kibaki akiwania urais na kupata ajali, alikuwa naye karibu huko mpinzani wake katika uchaguzi huo, Ruto akiwa hajulikani mahali alipokuwa.

Agosti 20, mwaka huu, Mahakama ya Rufani ya Kenya ilifutilia mbali mabadiliko ya katiba 'yaliyopigiwa debe' kwa pamoja na Rais Kenyatta na Raila Odinga.

Mtazamo wa wawili hao waliokuwa wapinzani wa kisiasa kabla ya kushikana mkono Machi 9, 2018 ulikuwa tofauti na ule wa Ruto na washirika wake, hivyo kuyafanya maamuzi ya mahakama hiyo kuwa yenye 'kuubeba' upande wa Ruto.

Mabadiliko yaliyopendekezwa na Mpango wa Maridhiano (BBI) ni pamoja na kungemwezesha mrithi wa Kenyatta baada ya uchaguzi mkuu kuwateuwa wabunge wa kuchaguliwa kuingia kwenye baraza la mawaziri.

Katiba ya Kenya ya mwaka 2010 ilizuia wabunge kuwa mawaziri na Rais Kenyatta akawa katika mkakati wa kuhakikisha wanasiasa hao wanaingizwa serikalini. Haikuwa hivyo.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2017, dalili za Rais Kenyatta kuwakumbuka kwa vyeo washirika wake zilionekana baada ya kuunda wadhifa wa Katibu Tawala Mkuu kwenye wizara na aliwateuwa, miongoni mwa wengine, wanasiasa walioshindwa katika uchaguzi huo.

Kuna wakati mkakati wa kumdhibiti Ruto ulishika kasi, ukiwamo wa makatibu tawala wakuu wa wizara kadhaa, kumshambulia kwa ukiukwaji wa kanuni za utumishi wa umma.

Wakati hayo yakitokea, serikali ya Kenyatta ilipiga marufuku mikutano ya hadhara kutokana na hofu ya kuenea kwa COVID- 19, hivyo ilimpasa Ruto kuyatumia makazi yake yaliyopo Karen, kufanya mikutano na watu wa kada tofauti wakiwamo wafuasi wake.

Pia Ruto alitumia misiba na nyumba za ibada kupenyeza ujumbe wa kampeni zake kwa Wakenya.

## BIBI TITI MOHAMED

# Alivyo 'jeshi kubwa' lakini taarifa zake hazifahamiki

- Rais Samia ataka zikusanywe, ziandikwe kumuenzi shujaa

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa RUFIJI**

OKTOBA 23, mwaka huu ilikuwa siku ya pekee kwa wakazi wa Ikwiriri wilayani Rufiji mkoa wa Pwani. Ni pale walipokusanyika kushuhudia tukio la kihistoria, si kwao tu, bali pia kwa Watanzania wote, wakati Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa CCM ulipofanya maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Wanawake.

Tukio hilo lingekuwa la kawaida kama lingefanyika mahali pengine, lakini hatua ya kuichagua Rufiji kama eneo maalum kwa maadhimisho hayo mwaka huu, pamoja na dhima ya kumbukizi ya Bibi Titi Mohammed, mwasisi wa UWT linaongeza upekee wa siku hiyo.

Kumbukizi hiyo inayofanyika kwenye Viwanja vya Ujamaa, inabeba maana kubwa kwa historia ya Tanzania, kwani mbali ya kuwa mbunge wa kwanza mwanamke wa kuchaguliwa akiiwakilisha Rufiji, Bibi Titi ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa kwanza wa UWT tangu umoja huo ulipoanzishwa mwaka 1955 na Chama cha TANU.

Ni kupitia Bibi Titi harakati na mchango wa wanawake katika kudai Uhuru wa Tanganyika zilijidhihirisha kiasi cha kuvuka mipaka ya nchi.

Pamoja na historia hiyo, tukio hilo la Rufiji linaongezewa upekee kutokana na kuwapo kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alikuwa mgeni rasmi, anayemtaja Titi kuwa ni mwanamama shupavu anayepaswa kuigwa.

Katika hotuba yake, anawahimiza viongozi kufuata nyayo zake kama shupavu na kinara wa kupigania uhuru wa nchi na kutetea maslahi ya wanawake.

"Licha ya mchango wake mkubwa kwa taifa na Afrika, mambo mengi ya Bibi Titi hayajulikani. Shujaa huyu, aliyezaliwa Juni 1926 jijini Dar es Salaam kwa wazazi Mohamed na mama Hadija waliotokea Rufiji, waliokuwa wakiishi Mzizima, hakuna mambo mengi kumhusu yanayojulikana." Anaongeza.

Rais Samia anatoa rai kuandikwa taarifa kuhusu mama huyo wa shoka katika siasa za ukombozi ili ziweze kufahamika kwa kuwa alifanya mambo makubwa ya kishujaa.

"Mambo hayo makubwa ya kishujaa aliyoyafanya ndiyo msingi wa hamasa ya ushiriki wa wanawake katika siasa za harakati za ukombozi wa Tanganyika, anasema." Na kuongeza:

"Bibi Titi alifanikiwa kwa kushirikiana na viongozi, akiwamo Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Rajab Diwani, kwa kiasi kikubwa kuwashawishi wanawake na wanaume kuungana naye katika harakati za kudai uhuru."

Anasema Titi, akiwa kiongozi wa wanawake wa TANU alitembea nchi nzima kuwahimiza kinamama kujiunga na chama hicho.

"Huyu ndiye mwanamke wa kuigwa na ningependa wanawake wote kuiga matendo na dhamira yake. Mwanamke alitakiwa tu kuonekana lakini siyo kusikika kwa sababu kwa wakati ule sauti yake haikuruhusiwa kuvuka ukuta wa nyumba yake," anakumbusha Rais.

Anaongeza: "Hatuwezi kuzungumzia harakati za Baba wa Taifa za kudai Uhuru wa Tanganyika bila kumtaja Titi, katika kipindi cha mpito cha kuelekea kwenye Uhuru, mwanamama huyu alikuwa mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGICO) akiwa peke yake alipaza sauti kuhimiza maendeleo vijijini wanapoishi wanawake wengi hata leo."

Anakumbusha kuwa, baada ya uhuru huo, Titi alikuwa mbunge na Naibu Waziri na aliendelea kupaza sauti yake katika kutetea maslahi ya wanawake na kuhimiza uwepo wa fursa sawa kati ya wanawake na wanaume kwenye ajira, elimu na afya huku akitumia muda mwingi kusukuma agenda ya haki za mtoto wa kike.

"Tukumbuke wakati Bibi Titi akiyafanya hayo hata vuguvugu la kudai haki za wanawake katika nchi za Magharibi halijapamba moto, hivyo maono ya mpendwa wetu huyu kutetea na kupigania haki za mwanamke yalitangulia ya nchi za kimagharibi ambazo kwa sasa zinaonekana mabingwa wa kutetea haki hizo," anasema Rais.

Anataja sifa nyingine ya Titi kuwa ni mwanamke mwenye msimamo na kujiamini na suala la jinsia halikumfanya aache kujiamini, alikuwa mtu wa kufanya kile analichoamini ni sahihi.

"Tukio kubwa linalotukumbusha ujasiri huu ni pale alipokataa kuunga mkono Azimio la Arusha na kuamua kuachia vyeo vyote alivyokuwa navyo kwa wakati huo, na mengine yaliendelea... huyo ndiye Titi Mohamed mwana wa Rufiji, mchango wake katika harakati za ukombozi za mtu mweusi kutoka katika makucha ya wakoloni ni mkubwa japo hajaandikwa vya kutosha," anasema.

### MASWALI MAGUMU UWT

Rais Samia anasema wanapoadhimisha kumbukumbu ya Bibi Titi wajiulize maswali haya, wanayafuata yale aliyokuwa anayafanya wakati huo?

"Sisi tuliopo leo tunayaishi aliyoyatetea na kuyaishi shujaa wetu huyu? Tunaendana na yale aliyofanya shujaa wetu huyu? Ni wangapi miongoni mwetu tunaweza kubeba ajenda ya ukombozi wa mwanamke kwa ujumla na kutokukubali kutumiwa kwa maslahi binafsi ya wakubwa ama ya watu wengine?" Anahoji Rais Samia.

Anaongeza: "Tumefanya jitihada zozote kuhakikisha ukombozi wa mwanamke kudai haki za watoto wa kike unaonekana? Ni wangapi miongoni mwetu wana ujasiri na moyo wa dhati wa kuwaunganisha wanawake wa Tanzania ili wafikie lengo la ukombozi kifikra, kisiasa na kiuchumi... ni wangapi?" Anahoji.

Rais Samia anasema, alipouliza maswali hayo hakumaanisha kupata majibu katika maadhimisho hayo, bali iwe ni tafakari kwao na waende kuyatakari kila mmoja kupitia taasisi zao na kupata majibu.

Anasema, watu walikusanyika kumsifu shujaa wao, lakini sifa hizo zisiwe kilemba cha ukoka bali wamsifu na wakiondoka katika eneo hilo wajuwe kuwa wanakwenda kujipanga na maono, matendo na dhamira ya shujaa wao.

### ILIPO HISTORIA YA TITI

Abdallah Mohammed ni mwanakijiji cha Mkongo, anasema kijijini hapo wameweka mnara kwa ajili ya kumbukumbuka Bibi Titi kutokana na harakati zake za ukombozi.

"Kikubwa tunakikumbuka kwa Titi wakati akiwa kiongozi alishawishi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Dar es Salaam hadi Kibiti na mengine mengi ," anasema Mohamed.

Anakumbusha kuwa alimshawishi Mwalimu Nyerere kufanya Mkutano Mkuu wa Halmashauri ya Taifa ya TANU kijijini hapo mwaka 1970.

"Kuna mnara mwingine umewekwa wa kumbukizi ya Mkutano wa Halmashauri ya Taifa ya TANU uliofanyika mwaka 1970, ulizinduliwa na Mkongea Ali, kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Julai 26, 2019," anasema.

Wana Rufiji wanamkumbuka Titi kwa sababu alikuwa jasiri asiyeogopa na alisimamia maendeleo ya nchi akishirikiana na Mwalimu Nyerere katika harakati za kuleta uhuru.

"Titi alikuwa jasiri aliyejitoa muhanga kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi hii, ndiyo maana tumemjengea mnara hapa kijiji kwetu," anasema na kuongeza kuwa kinachoonekana leo nchi ikiongozwa na mwanamke ni kielelezo cha ndoto zake kutimia.

Anasema, Rais Samia anawateua wanawake mbalimbali kushika nafasi serikalini, jambo ambalo ni moja ya ndoto alizokuwa anazipigania Bibi Titi.




Mnara wa kumbukumbu ya Bibi Titi, ulioko kijijini Mkongo wilayani Rufiji. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# SUDAN YAMKINI SI SHWARI TENA

## ■ Abdel Fattah al-Burhan, anairudisha rasmi kwenye udikteta
## ■ Hamdock, baraza la raia, jeshi vyawekwa pembeni



Kiongozi wa mapinduzi wa Sudan Abdel Fattah al-Burhan.



Waziri Mkuu, Abdalla Hamdock, aliyenusurika kifo mwezi uliopita sasa amewekwa pembeni na jeshi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

SUDAN ni nchi ya tatu kwa ukubwa barani Afrika, iliyo na migogoro ya uongozi huku ikirekodi majaribio kadhaa ya mapinduzi na hivi karibuni Waziri Mkuu Abdalla Hamdok, akinusurika kuuawa kwenye shambulio la bomu nyumbani kwake jijini Khartoum.

Baadaye kupitia taarifa za mtandao wa twitter akielezwa kuwa Waziri Mkuu yuko salama. Hamdok aliyeteuliwa kuongoza serikali ya mpito, Agosti 2019, baada ya kiongozi wa muda mrefu, Omar al-Bashir kuondolewa madarakani na majeshi kufuatia miezi kadhaa ya maandamano ya kuupinga utawala wake.

Hamdok mwezi uliopita aliponea chupuchupu, kwenye shambulio lilitokea baada ya bomu kupiga gari lake, lakini hakukuwa na vifo wala majeruhi, baadaye mitandao ikaeleza kuwa yuko salama licha ya kwamba ameondolewa kwenye uongozi.

Vyombo vya habari vinaeleza shambulio hilo kutokea karibu na kaskazini mashariki liliko daraja la Kober, ambalo linaunganisha eneo la kaskazini na jiji la Khartoum. Wakati hayo yakitokea vikosi vinavyotaka demokrasia vilitoa wito kwa watu kufanya maandamano makubwa mwishoni mwa juma kuonyesha nia yao ya kuendelea kulikaidi jeshi.

Jeshi la Sudan lilitwaa mamlaka na kumkamata Waziri Mkuu Hamdock na mawaziri kadhaa katika mapinduzi kwa siku chache, kisha kumwachilia huru kiongozi huyu anayelaumiwa kwa kusababisha kudorora uchumi na maisha ya watu.

Mapinduzi hayo yamemaliza kipindi cha utawala wa pamoja wa jeshi na vikosi vinavyounga mkono demokrasia tangu kusambaratika kwa serikali ya kiimla mwaka 2019, na katika mji mkuu wa nchi hiyo, Khartoum, waandamanaji waliingia mitaani kupinga mabadiliko.

**MAPINDUZI**

Kiongozi wa mapinduzi Sudan, Abdel Fattah al-Burhan, baada ya mapinduzi alifahamu kwamba ni chanzo cha kutengwa na jumuiya za kikanda na kimataifa, ikiwamo kuondolewa misamaha muhimu ya madeni na misaada ya kimataifa iliyokuwa imeahidiwa.

Marekani imesitisha msaada wa dola milioni 700 na mpango wa kusamehewa deni lilitokana na makubaliano na jitihada za Hamdok. Abdel Fattah, aliyekuwa mkuu wa baraza huru la Sudan na jeshi kwenye serikali ya pamoja ya jeshi na raia hadi ametwaa madaraka yote.

Baada ya kuvunja baraza la mawaziri la raia, anamkamata Waziri Mkuu Abdalla Hamdok na watu wengine mashuhuri ambao jeshi lilikuwa limeafikiana nao kugawana madaraka hadi wakati wa uchaguzi mwakani.

Anaonyesha wazi kutokuwa na uvumilivu na uongozi wa Hamdok, akiwa kama mtawala mwenye nguvu kijeshi, aliona anahitaji kuiokoa nchi hiyo.

Wakati wa maandamano ya hivi karibuni, yaliyoungwa mkono na jeshi kwenye Mji Mkuu Khartoum, waandamanaji walimlaumu Hamdok kwa kudorora viwango vya maisha.

**KAULI ZA WADAU**

Chama cha Wasomi Sudan kilichoongoza maandamano yasiyo yenye ghasia yaliyoangusha utawala wa miaka 30 ya Omar al-Bashir mwaka 2019, walijiandaa kwa awamu mpya ya maandamano mitaani.

Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Mataifa (UN) na Shirika la Maendeleo la Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika (IGAD) na wafadhili wote wa Sudan wa nchi za magharibi walilaani mapinduzi hayo na kutoa wito wa kurudi kwenye utawala wa kiraia.

Saudi Arabia na Milki ya Nchi za Kiarabu walitoa msaada muhimu wa kifedha kwa Gen Burhan mwaka 2019 hawakusema neno lakini Jeneral Burhan tayari alikuwa mtu mwenye nguvu zaidi nchini humo na nafasi yake ilihalalishwa na makubaliano ya kugawana madaraka ya mwaka 2019 kati ya jeshi na makundi ya raia ya 'Forces for Freedom and Change -FFC.'

Kulingana na makubaliano hayo, Gen Burhan angeng'atuka kama mwenyekiti wa baraza huru mwishoni mwa mwaka huu.

Wakati huo raia ambaye angeteuliwa na FFC angekuwa kiongozi na raia serikalini wangekuwa na nafasi nzuri ya kutekeleza yaliyokuwa kwenye ajenda zao. Moja ya ajira ni uwajibikaji kwa ukiukaji wa haki za binadamu. Serikali ilijitolea kumsalimisha rais wa zamani Omar al-Bashir kwenda mahakama kimataifa ya uhalifu wa kivita ICC nchini Uholanzi.

**ANACHOPINGA HAMDOK**

Hamdok amekuwa akilikosoa jeshi kwa kuingilia uchumi, jeshi linasimamia mgawo mkubwa wa bajeti, kampuni zinazomilikiwa na jeshi hazilipi ushuru na zimetuhumiwa kuhusika na ufisadi. Hata hivyo kuliweka jeshi chini ya udhibiti wa raia ilikuwa ajenda kwa awamu ambayo ingefuatia ya kipindi cha mpito.

Baada ya mapinduzi hayo yaliyofanyika mwezi uliopita, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ((UN), António Guterres, anaeleza kushtushwa kwa shambulizi hilo na kwamba yuko pamoja na Waziri Mkuu na watu wa Sudan.

Umoja wa Mataifa na Muungano wa Afrika wa Kulinda Amani Darfur, (UNAMID), ulitoa taarifa ya ukieleza masikitiko yake kuhusu jaribio hilo la mauaji. Wakati hayo yakitokea intaneti na mitandao ya kijamii imefungwa kwa kiwango kikubwa, wanajeshi wamewafyatulia risasi waandamanaji na kuripotiwa kuua watu 10.

Wanaharakati wameshinda hatua kama hizo awali na kulazimisha jeshi kulegeza kamba hasa baada ya mauaji ya Juni 2019. Makubaliano ya amani mwaka uliopita yaliyaleta makundi kadhaa yenye silaha ndani ya serikali, japo hadi sasa hakuna makubaliano yaliyofikiwa na makundi mawili makubwa ya waasi. Huko Darfur kuna kundi la Sudan Liberation Movement linaloongozwa na Abdel Wahid al-Nur, na katika milima ya Nuba, Kordofan Kusini lipo kundi la Sudan People's Liberation Movement-North, linaloongozwa na Abdel Aziz al-Hilu, bado makubaliano hayajafikiwa.

Mwaka 2019 kufuatia harakati mbaya za jeshi kwa makundi ya waandamanaji, Marekani, Uingereza, Saudi Arabia na Falme za Kiarabu walishinikiza kuwapo suluhu kwa njia ya mazungumzo suluhu iliyopatikana mwezi uliofuatia.

**MAANDAMANO**

Watu kadhaa waliripotiwa kufariki dunia wakati wa maandamano ya kuunga mkono demokrasia, katika mji mkuu wa Sudan Khartoum, maandamano mapya ya kuunga mkono demokrasia yalifanyika, Jumamosi iliyopita wiki tatu baada ya mapinduzi ya kijeshi ya Jenerali Abdel Fattah al-Burhan.

Hali ni ya wasiwasi katika maeneo kadhaa ya mji mkuu wa Sudan Khartoum, huku watu watano miongoni mwa waandamanaji wakiripotiwa kufariki dunia baada ya kupigwa risasi. Waandamanaji wengine wameuawa mjini Khartoum Jumamosi iliyopita na kufikisha idadi ya watu watano kutoka kambi ya upinzani wa mapinduzi waliouawa kwa kupigwa risasi na kurushiwa mabomu ya machozi na vikosi vya usalama, chama cha madaktari wanaounga mkono demokrasia umesema.

Maelfu ya Wasudani wanaendelea kupiga kelele "hapana kwa utawala wa kijeshi" katika mitaa ya Khartoum na miji mingi nchini Sudan wakati wa maandamano nchini humo dhidi ya mapinduzi yaliyoongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhane.

"Watu wengi wamejeruhiwa kwa kupigwa risasi katika maeneo tofauti ya Khartoum", chama cha madaktari wanaounga mkono demokrasia kinad na kuarifu kuwa takriban waandamanaji 20 wameuawa tangu Oktoba 25, mwaka huu, huku vyombo vya usalama vikitumia gesi ya kutoa machozi maeneo kadhaa ya Khartoum.

**MITANDAO**





## CRDB kukopesha mabilioni kiwanda

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya CRDB imeonyesha nia ya kutoa Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya kufufua mradi wa kiwanda cha mawese cha Trolle Meesle Tanzania Limited cha kuchakata kilichopo eneo la Sido mkoani Kigoma.

Serikali imeanza mazungumzo na Benki hiyo ili kuona namna ya kukifufua kiwanda hicho.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alilolitoa kwa Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, eneo la Sido mkoani Kigoma,

Hayo yalisemwa jijini hapa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe baada ya kumaliza mazungumzo yake na wadau mbalimbali wa mradi huo akiwamo mmiliki wa Kitanzania ambaye amewekeza Sh. milioni 450 na dhamana ya nyumba na shule ili kuanzisha mradi huo.

Alisema katika ufadhili huo, CRDB imeonyesha dhamira ya kukubali kufadhili wakulima ambao wataingia kwenye chama cha ushirika (AMCOS) na kupata fedha za kuendeleza kilimo cha michikichi yao.

Bashe alisema mradi huo ambao ulikwama ni wa miaka 6 ambao uko chini ya Kampuni ya Primaslii, mradi ulifadhiliwa na Ubalozi wa Denimark kupitia shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (Danida) kwa kushirikiana na serikali, ulikamilika mwaka 2019, na baadae TIDB na Danida walikubaliana kufadhili mradi huo wa kiwanda hicho katika mkoa wa Kigoma.

Aliafafanua kuwa katika uwekezaji wa kiwanda hicho, asilimia 70 ya ununuzi wa vifaa za kiwanda zilifadhiliwa na Danida, huku asilimia 30 zikitolewa na mwekezaji binafsi na kwamba waliweka makubaliano ya kisheria katika uwekezaji huo na kiasi cha Sh. milioni 450.

**Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alilolitoa kwa Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, eneo la Sido mkoani Kigoma,**

# CBE yaitisha mkutano kupokea, kujadili utafiti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kimeandaa mkutano wa kitaaluma wa siku mbili wenye lengo la kuwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti unaofanywa na wataalamu kutoka ndani na nje ya nchi.

Makamu Mkuu wa chuo hicho (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu), Prof. Tandi Lwoga, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkutano huo.

"Huu ni mkutano wa pili ukitanguliwa na ule uliofanyika mwaka jana jijini hapa, mkutano wa mwaka huu unaenda na dhima iitwayo 'Ukuaji wa Uchumi kwa Maendeleo Endelevu,' alisema Pro. Lwoga.

Alisema, mbali na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti vilevile kutakuwa na uwasilishaji wa mada mahsusi zinazahusu uchumi na biashara kwa maendeleo shirikishi.

"Mada hizo zitatolewa na Prof. Honest Ngowi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Alfred S Sife (MOCU), na Mheshimiwa Jumanne Kishimba (Mbunge) wengine ni Maida Waziri , mjasiriamali, Godfrey Nyaisa kutoka Brela na wengine wengi," alisema.Kadhalika, alisema mkutano wa mwaka huu utafunguliwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dk. Stergomena Tax.

Aidha, alisema mkutano huo utahudhuliwa na watafiti kutoka ndani na nje ya nchi, wafanyabiashara na wanazuoni zaidi ya 300.

"Katika mkutano huu matokeo ya utafiti zaidi ya 80 yatawasilishwa ambapo utafiti wa mwaka huu umejikita katika maeneo ya ubunifu na ujasiriamali, uchumi na maendeleo endelevu, fedha na biashara, uchumi wa kidijitali, biashara za kimataifa, TEHAMA na biashara ,elimu ya biashara na fursa za uwekezaji," alisema.

Alisema, faida za mkutano huu wa kitaaluma ni kuibua fursa za biashara na kiuchumi na washiriki kuongeza mtandao kwa kukutana na watu wenye nia sawa.

"Faida nyingine ni kupanua maarifa na kupata suluhisho la matatizo na kupata mbinu mpya na taarifa ambayo haijachapishwa, watapata taarifa za utafiti mkubwa pamoja na wawasilishaji wenye majina makubwa katika maeneo yao,"alisema.

Vilevile, alisema mikutano ya kitaaluma ni njia nzuri ya watu kukutana na wenzao bila kujali vyeo vyao, taaluma zao na mataifa yao.

"Sisi kama chuo ili kuenzi mambo yetu na kuhakikisha matokeo ya tafiti hizi yanawafikia walengwa wengi zaidi tumeamua kutumia lugha adhimu ya Kiswahili ili kuenzi lugha yetu," alisisitiza.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (wapili kulia), akizungumza wakati akizindua Bodi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Naibu Waziri wake, Deogratius Ndejembi, Naibu Katibu Mkuu, Dk. Francis Michael (wapili kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi, Sophia Kaduma. **PICHA: UTUMISHI**

# Waziri apigia debe mikopo kwa wanafunzi wa VETA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeiagiza Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuangalia namna ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wanajiunga na vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) na vya maendeleo ya jamii.

Lengo ni kuwawezesha waende kuisaidia serikali katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa.

Aidha serikali imeagiza kuanzia juzi ajira zote zinazoombwa zifanyiwe kazi na Sekretarieti ya Ajira na ili kupunguza rushwa, ukabila, udini na undugu ambao ulisheheni katika taasisi mbalimbali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi

wa Umma na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa, alibainisha hayo juzi wakati akizindua Bodi ya Sekretarieti ya Ajira, jijini Dodoma.

Waziri Mchengerwa alisema ni vyema Bodi ya Mikopo ikaliangalia suala la utoaji mikopo katika vyuo vya VETA na Maendeleo (FTC) ambavyo vinatengeneza wahitimu wanaokwenda kujiajiri wao wenyewe na kuipunguzia serikali mzigo.

Alifafanua kuwa vyuo hivyo vilianzishwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambavyo miaka ya nyuma vilisaidia kupunguza mzigo wa ajira serikali, hivyo na wao wanapaswa kuvijali na kuwajali wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo hivyo.

Akizungumzia kuhusiana na ajira zote kupitia Sekretarieti ya Ajira Mchengerwa alisema hivi sasa ajira zote zitapitia katika sekretarieti hiyo ili kupunguza rushwa, ukabila, udini na undugu ambao ulikithiri katika baadhi ya taasisi na idara mbalimbali za serikali.

Aliitaka Sekretariati ya Ajira kupitia Katibu Mkuu na Naibu wake kwenda kuliondoa hilo ili kuweka uwazi wakati wa kutoa ajira.

"Kuna baadhi ya taasisi zilianza kuajiri wenyewe, naomba hili jukumu lichukuliwe na wizara na lifanyiwe kazi kwa uwazi na usawa," alisema Mchengerwa.

Mchengerwa aliwataka wakuu wa Wilaya na Mikoa kuhakikisha wanatengeneza ajira binafsi kupitua fursa za serikali zinazotolewa katika maeneo hayo ili kuwasaidia wananchi.

Alisema wakuu hao wanapaswa kutumia miradi ya kimkakati na TASAF ili kutengeneza ajira na kuondoa umaskini kwa wananchi.

Aliwataka pia kuangalia baadhi ya taasisi ambazo watumishi wanalipwa bila kufanya kazi yoyote kutokana na halmashauri kuwa na watumishi wengi wakati halmashauri nyingine hazina watumishi.



# Asasi hatarini kufutwa kutohuisha usajili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI inakusudia kufuta usajili wa asasi zote za kijamii nchini ambazo zitashindwa kuhuisha vyeti vyao vya usajili ifikapo Novemba 30, mwaka huu.

Msajili wa Asasi za Kijamii katika Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi, Emmanuel Kihampa, alisema hayo juzi wakati akizindua uhuishaji vyeti vya usajili vya asasi za kijamii mkoani Mbeya.

Alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa sheria za usajili wa asasi za kijamii na kwamba kwa sasa kazi hiyo inazihusu taasisi zisizo za kidini.

"Tumebakiwa na siku 15 tufunge usajili wa asasi za kijamii. Naomba muda uliobaki utumiwe vizuri kwa kufika katika ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Mbeya kwa wakazi wa Mkoa wa Songwe na Mbeya, Rukwa na Katavi na Iringa wananchi wa Njombe wafike ili kuhuisha vyeti vyao au kusajili kama hawakufanya hivyo," alisema Kihampa.

Alisema miongoni mwa asasi zinazotakiwa kusajiliwa au kuhakikiwa taarifa zao ni pamoja na vikundi vya kuinua kiuchumi, vikundi vya kitaaluma na kikanda.

Pia alisema miongoni mwa faida za usajili na uhakiki wa taarifa za vikundi vya kijamii ni kuisaidia serikali kufahamu uhai wa asasi hizo ili kupatiwa mahitaji sawasawa na zilizovyasajiliwa.

Alisema kazi hiyo inafanyika kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1955 na kwamba ni miaka 66 sasa jambo ambalo linahitaji umakini na kufahamu idadi ya vikundi vilivyo hai hadi sasa.

Mkoa wa Mbeya una asasi 300 ambazo zinajumuisha za kidini na zisizokuwa za kidini na kwamba mchakato wa kubaini idadi ya makanisa yaliyoko mkoani humo unaendelea huku zoezi la kuhuisha vyeti vya usajili wa asasi za kijamii likifanyika kwa siku tatu mfululizo mkoani humo.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akizindua ujenzi wa vyumba vya madarasa 636 vya mpango wa maendeleo wa Taifa na mapambano dhidi ya Uviko 19, jijini Mbeya juzi. (Wapili kulia) ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya mjini, Dk. Tulia Akson. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbunge ahimiza uhuru, demokrasia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, amewaomba viongozi kuendelea kudumisha uhuru na demokrasia iliyoasisiwa na Hayati Mwalimu Julius Nyerere ili mwananchi awe huru kuchagua chama cha kisiasa anachokitaka.

Mwakagenda alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na Nipashe juu ya mtazamo wake kuelekea miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema yako mengi ya kujivunia na yaliyofanywa na Hayati Nyerere ikiwamo kulikomboa taifa dhidi ya wakoloni na kuhimiza ujamaa na kujitegemea.

"Tunajivunia kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa imetusaidia kuwa huru kuchagua vyama tunavyovitaka licha ya kupitia vipindi mbalimbali lakini bado tunaendelea kuwaomba viongozi walioko madarakani kutekeleza haki na demokrasia," alisema Mwakagenda.

Mwakagenda aliiomba serikali kusimamia haki ili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, aachiwe huru na kuendelea na majukumu yake ya kulijenga taifa.

Alisema uhuru wa kujieleza na kutoa maoni ni muhimu ukaheshimiwa bila kujali itikadi za kisiasa na kusisitiza utu na uzalendo katika kujenga nchi.

Hivi karibuni, mwanahabari mkongwe nchini, Jenerali Ulimwengu, akiwa mkoani Mbeya wakati wa kongamano la katiba aliwahamasisha Watanzania kuwa majasiri katika kuhoji utendaji kazi wa viongozi waliowachagua katika maeneo yao hususani madiwani na wabunge.

Alisema kwa kufanya hivyo kutaongeza uwajibikaji na kushirikishwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kuliko ilivyo sasa wamesahau wajibu wao kwa wananchi hadi wakati wa uchaguzi utakapowadia ndipo wataanza kuwabembeleza.

Pia alisema katiba mpya ndiyo suluhisho la kutetea haki za wananchi na kuongeza uwajibikaji baina ya viongozi na wananchi kupata maendeleo.

## Walia na utitiri wa vyama vya wafanyakazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi wameiomba serikali kufanya marekebisho ya sheria ili kupunguza idadi ya vyama vya wafanyakazi.

Wamesema wingi wa vyama hivyo hauwasaidii wafanyakazi kutetea maslahi yao na badala yake unazidi kuwadidimiza.

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walisema hayo jana wakati wakizungumza na Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini, Pendo Berege, alipotembelea Chuo cha Wafanyakazi (OTTU), kilichoko jijini Mbeya.

Rose Lamosai, Mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi wa Afya na Serikali Kuu (TUGHE) mkoa wa Mbeya, alisema ni muhimu wafanyakazi kuungana kwa pamoja kuimarisha chama kimoja ambacho kitatetea maslahi yao kuliko kugawanyika na kuanzisha migogoro.

"Wingi wa vyama vingi haimaanishi kuwa wamoja badala yake tunatengeneza migogoro naomba tuweke nguvu kuimarisha umoja wetu ambao unatuunganisha watumishi wote na kutetea maslahi yetu," alisema Lamosai.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha OTTU, Martha Lwitiko, aliwataka viongozi wa vyama vya wafanyakazi kujenga uhusiano mzuri mahali pa kazi ili kuepusha migogoro miongoni mwa wafanyakazi na waajiri.

Berege alisema Sheria ya usajili wa Vyama vya Wafanyakazi inaweza kubadilishwa endapo mchakato huo utaanzia kwa wafanyakazi wenyewe.

Alisema wingi wa vyama vya wafanyakazi unadaiwa hausaidii kutetea maslahi ya mfanyakazi na badala yake unazidi kuwadidimiza, hali ambayo imesababisha baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kuiomba serikali ifanye marekibisho ya sheria kwa lengo la kupunguza idadi ya vyama vya wafanyakazi nchini.





## Wawakilishi wataka makandarasi waadilifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imeitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha wanatafuta makandarasi wenye uwezo na waaminifu katika miradi mikubwa ili kuepuka hasara.

Akizungumza jana wakati wa kikao cha kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mpango wa elimu kwa kipindi cha robo ya Julai-Septemba 2021/2022 katika ukumbi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwantatu Mbarak Khamis, alisema kumekuwapo ubabaishaji kwa badhi ya makandarasi wakati wa ujenzi wa miradi, hali inayopelekea kuchelewa kwa ujenzi wa majengo kwa mujibu wa mkataba ulivyokusudiwa.

Pia, aliitaka Wizara kuwa na umakini kwa makandarasi kwa kuepuka gharama kubwa hasa wanapojenga miundombinu hiyo katika maeneo ya visiwa pamoja na kuwa makini katika ufuatiliaji wa miradi hiyo kwa ukaribu zaidi.

Hata hivyo kamati hiyo kupitia mwenyekiti, aliitaka Wizara ya Elimu kuwasimamia walimu katika utendaji wao wa kazi ili kupunguza tatizo la kufeli kwa wanafunzi, pamoja na kuwafuatilia katika mahudhurio yao.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mpango wa elimu kwa kipindi cha robo ya Julai-Septemba 2021/2022, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, alisema Wizara yake imekusanya jumla ya Sh. milioni 90 ambapo imekiuka shabaha iliyojiwekea ya kukusanya Sh.milioni 42, 475,500.

Alisema makusanyo hayo yamekusanywa katika kipindi cha robo mwaka ambapo ongezeko la makusanyo hayo yametokana na ukusanyaji wa chanzo kipya cha mapato, ambacho ni malipo ya mitihani ya shule za binafsi pamoja na malipo ya leseni za walimu na usajili wa shule binafsi.

Simai alisema fedha hizo zimetumika katika masula mbalimbali ya kuimarisha masuala ya elimu katika nyanja mbalimbali.

Alisema pamoja na wizara hiyo kukusanya fedha hizo, lakini bado ina changamoto ya bajeti na hiyo inapelekea kusuasua kwa baadhi ya utekelezaji wa majukumu yake.

# Mwinyi ataka biashara ya pamoja Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka nchi za Bara la Afrika kuhakikisha zinafanya biashara ya pamoja badala ya kuelekeza nguvu zaidi nje ya bara hilo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika hotuba yake aliyoitoa kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Maonyesho ya Biashara baina ya nchi za Afrika, unaofanyika Durban, Afrika Kusini ambapo amemuwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Mwinyi alisema kuwa ili kufikia azma iliyokusudiwa, ni muhimu kutekeleza malengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa eneo huru la Biashara Afrika (AfCFTA) ambapo katika utekelezaji wake alihimiza haja ya nchi wanachama wa AfCFTA kushirikiana katika kuzifanyia kazi changamoto zilizopo, ambazo ni kikwazo kwa maendeleo ya biashara na uwekezaji.

Alizitaja miongoni mwa changamoto zinazozifanya nchi za Afrika zishindwe kufanya biashara baina yao kutokana na kukabiliwa na vikwazo vingi vinavyosababisha kiwango cha biashara kuwa ndogo baina yao pamoja na ufinyu wa miundombinu kati ya nchi zenyewe, utatanishi uliopo kuhusu viwango vya ushuru, migongano ya sheria na uhaba wa bidhaa zinazozalishwa.

Rais Dk. Mwinyi alisisitiza kwamba lengo la mkutano pamoja na maonyesho hayo ya Biashara ni kuimarisha uhusiano wa kibiashara baina ya nchi za Afrika hivyo, kuna kila sababu ya kutiliwa mkazo na kufanyiwa kazi ipasavyo azma hiyo.

Aidha, alieleza kwamba kiwango cha kufanya biashara baina ya nchi za Afrika bado ni kidogo mno na badala yake sehemu kubwa ya biashara inafanywa katika nchi zilizoendelea zikiwamo za Ulaya na Marekani.

Marais na viongozi kutoka nchi mbalimbali waliohudhuria mkutano huo walipata fursa ya kueleza mikakati na juhudi zinazochukuliwa na nchi zao katika kuhakikisha suala zima la biashara huria linapewa kipaumbele katika Bara la Afrika ili maendeleo zaidi yaweze kupatikana huku wakieleza athari za UVIKO 19 zilivyorejesha nyuma hatua hiyo.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ambaye ndiye mwenyeji wa mkutano huo, alieleza utayari kwa nchi hiyo katika kutoa ushirikiano juu ya suala hilo.



Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), akipokea hati kutoka kwa Balozi mdogo wa China Zanzibar, Zhang Zhisheng jijini Zanzibar jana, ambapo serikali ya China inatarajia kuikabidhi dozi mpya 250,000 za chanjo ya UVIKO -19. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mama Mariam Mwinyi atabiria wanawake fursa uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZINAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, amesema kuna uwezekano mkubwa kwa wanawake kustawi katika uchumi wa bluu ikiwa usawa wa kijinsia utaboreshwa na wanawake wataunganishwa katika maeneo yote.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Dk Sada Mkuya Salum, aliposoma hotuba kwa niaba yake katika warsha ya fursa za uchumi wa bluu kwa wanawake ilioandaliwa na Shirika la Maendeleo la UN WOMEN. Warsha hiyo ilifanyika Mjini Zanzibar na kuzindua ripoti kuhusu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika uvuvi, uchumi wa bluu katika Bahari ya Hindi. Alisema kunahitaji mabadiliko ya sera na fikra, ili vikwazo vinavyozuia uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika sekta ya uchumi wa bluu ikiwa ni pamoja na sheria za kibaguzi, kanuni, mila na mitazamo hasi viondolewe.

Alisema wakati Zanzibar inatekeleza sera yake ya Uchumi wa Bluu, ni lazima kuhakikisha wanawake wanainuliwa kiuchumi na hawaachwi nyuma.

Aidha, alisema bado kuna changamoto kubwa za kimaendeleo zinazopaswa kushughulikiwa ili kuhakikisha kuwa wanawake wananufaika sawa na fursa za kiuchumi.

Alieleza kuwa ili kukabiliana na changamoto hizo, sera, mikakati na hatua mahususi zinatakiwa kushughulikia mahitaji mahsusi ya wanawake na wasichana na kuwezeshwa kutambua haki zao za kiuchumi.

Alieleza kuwa asilimia 32 ya kaya zinazoongozwa na wanawake Zanzibar zinafanya kazi katika sekta ya kilimo au uvuvi, na wanawake ndio wengi katika sekta ya utalii na ufugaji wa samaki, hivyo ni muhimu kuwezeshwa katika uchumi wa bluu.

"Kuna uwezekano mkubwa kwa wanawake kustawi katika uchumi wa bluu ikiwa usawa wa kijinsia utaboreshwa na wanawake wataunganishwa katika maeneo yote," alisema.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alipongeza UN WOMEN kwa mchango wao mkubwa katika kuunga mkono, kusaidia na kuimarisha ajenda ya uchumi wa bluu Zanzibar hasa katika kupigania na kuhakikisha haki na maslahi ya wanawake katika uchumi wa bluu yanashirikishwa na kutekelezwa kwa ukamilifu. Alieleza kuwa warsha hiyo ni muhimu katika kufanikisha mwendelezo wa juhudi za serikali katika kuhakikisha haki na usawa wa wanawake na na jamii kwa ujumla kufanikisha azma ya uchumi wa bluu hasa katika uvuvi na mazao ya baharini.

Mwakilishi wa UN WOMEN Hodan Addou, alisema mchango wa wanawake ni mkubwa katika mapato ya kaya na usalama wa chakula, kiuchumi katika kujipatia kipato, lakini bado kazi zao katika uvuvi inakosa kutambuliwa rasmi na wanawake hawajawakilishwa sana katika sera na kufanya uamuzi.

"Ikiwa tunataka kuboresha kikamilifu rasilimali za bahari zetu ili kukidhi mahitaji yetu ya maendeleo kwa njia endelevu, ikiwa ni pamoja na kuunda nafasi za kazi na kupunguza umaskini na ukosefu wa usawa, jukumu la wanawake haliwezi kupuuzwa," alisema.

Alisema hilo ni muhimu sana kwa Zanzibar, kwa sababu rasilimali na huduma za bahari zinajumuisha zaidi ya asilimia 37 ya Pato la Taifa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**HURBERT DICKSON MBUGI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0341-0633** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary SANGU mwaka 2012, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa CONTROL NAMBA **9910811394462**

---

JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA \ SHAURI LA RUFAA YA MADAI
NA. 22/2020
(Asilia kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya shauri la Madai Na.74 ya Mwaka 2013)

NIKO INSURANCE (T) LTD.......................................MRUFANI
DHIDI YA
1.YAHAYA BROWN MWANJOKA
(administrator of the estate of the late Asia Yahaya, Fatuma Bahati and Abubakari Matia)

2.CIPEX COMPANY LTD...................WARUFANIWA
3.ABDILAH BAKARI

KWA: ABDILAH BAKARI.
POPOTE ULIPO

**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA NA 3.**

Unataarifiwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya Tarehe 08/12/2021 siku ya Juma tano Saa3:00 Asubuhi,ambapo Shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe28 Mwezi OCTOBA,Mawka 2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI.

NDUGU **RWEGESILA VALENTINE MFUNGO** WA LAMAD BUSEGA SIMIYU ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA KADI ZAKE TATU ZA PIKIPIKI AINA YA **SUNLG MC429BTX,MC745CQN NA MC 541 CPS** TAARIFA IMETOLEWA KITUO CHA POLISI LAMAD BUSEGA SIMIYU,LAM/IR/1000/2020 YEYOTE ATAKAYEZIONA AWASILIANE NAYE KWA NAMBA 0774905844 AU KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICO MABOGA KANIAGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 698 AEA** chasis namba **FE537B502171** engine namba **4D33D50842,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MKB/RB/239/2021.**

---

JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MBEYA
\SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 155/2020
(Asilia Shauri la Jinai Na.246/2019 Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)
JAMHURI...................................MRUFANI
DHIDI YA
JOSEPH JUMA KYANDO..................MJIBU RUFAA
KWA BWANA: JOSEPH JUMA KYANDO.

POPOTE ULIPO.

**KUITWA SHAURIN.**

Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani, Tarehe 22/11/2021 siku ya Juma tatu Saa3:00 Asubuhi bila kukosa. ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 06 October,2021.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ADAM VITUS MAPUNDA** wa Magagura Songea anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.183/01** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **STELLA MATUTINA LUGHANO SEMINARY** mwaka **2002.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SO/RB/2021.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA
Kituo cha MWANG'OMBA Mkoa wa TANGA
KUITWA SHAURINI MSHITAKIWA
(Aya ya 9 Nyongeza ya 111 ya sharia ya Mahakama za Mahakimu)

Kwa: MARIAM OMARI
% M/K KWAHEZA

**Kwa kuwa imelazimika uhudhurie ili ujibu shtaka dhidi yako TSH. 4,500,000/=**

Unaamriwa na Mahakama uhudhurie mbele ya Mahakama hii tarehe 23 Mwezi wa 11 Mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi ili shauri liweze kusikilizwa. Endapo utashindwa kuhudhuria siku na muda uliopangwa hapo juu, na ikithibitika kwamba umepokea kuitwa shaurini, hati ya kukamatwa itatolewa dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi wa 11 Mwaka 2021.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANG'OMBE

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe
Kituo cha njombe mjini
Mkoa njombe
Usimamizi wa mirathina 105/2021
Katika shauri la mirathi ya
DENIS SULEMAN SAFARALI......marehemu wa njombe
Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na ALLY SELEMAN SAFARALI...muombaji

**TANGAZO KWA UMMA**

(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirthi mahakama ya mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23/11/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi .mapingamiziyoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla u mpaka tarehe tajwa hapo juu

Zingatia:endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 16/11/2021

HAKIMU MKAZI

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba kituo cha Kyaka Mkoa wa Kagera
Usimamizi wa Mirathi Na 19/2021
Katika Shauri la Mirathi ya Marehemu WILBARD RWEHUMBIZA BAJUNANA Wa Bugandika-Igurugati
Katika Shauri la Maombi ya Kuteua Msimamizi yaliyoletwa na HARUNA SAIDI KISHUGI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote masilahi yoyote na mirathi na marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili .Endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23,Mwezi 11 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi tajwa.

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 22/Octoba/2021

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KYAKA

---

IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY
(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)
AT TEMEKE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.14 OF 2021
In the matter of estate of the late ADON MUGETA KATONDO
And
In the matter of application for letters of administration by ALICE NYABINA MUNISI

**GENERAL CITATION**
(rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the letters of administration is made to the above named petitioner Objections to the grant should be filed on or before the 17th day of December 2021

Dated at ADAR ES SALAAM this 16th day of October, 2021

DEPUTY REGISTRAR

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KERRY WILLIAMS** MAKUNDE anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 759 DMD SUZUKI SWIFT.** Chassis namba **ZC31S201889.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAWE/RB/4994/2021.**

---

## MAJEMBE AUCTION MART LTD (VIJANA WA KAZI)

## TANGAZO LA MNADA WA MAGARI

Kwa niaba ya **K-FINANCE LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari la wadaiwa wanaotajwa hapo chini.

**Mahali:** Mwananyamala, Komakoma nyuma ya Biashara Complex

| JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| DAN NICK MTANGA | ANGELA ROBERT MCHOME | GARI AINA YA TOYOTA IST NAMBA YA USAJILI T 834 DHF | JUMANNE 23/11/2021 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Mnunuzi atalipa hela yote iliyoafikiwa kwenye mnada.
2. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi
3. Kwa maelezo Zaidi wasiliana nasi kwa simu namba **0738165605/ 0764525253/ 0715980025 na 0738165606.**

---

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MASJALA NDOGO YA TEMEKE
(TEMEKE KITUO JUMUISHA HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)
UTHITIBITHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
MIRATHI Na. 30 YA MWAKA 2021
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU:
REGINA MUTEMBEI RWEYEMAMU
MWOMBAJI: ALISON RICHARD MUTEMBEI NA ANDERS RICHARD MUTEMBEI
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 01 Mwezi wa Desemba, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10 Mwezi wa Novemba, 2021.**

NAIBU MSAJILI

---

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MASJALA NDOGO YA TEMEKE
(TEMEKE KITUO JUMUISHA HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)
UTHITIBITHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
MIRATHI Na. 30 YA MWAKA 2021
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU:
PROSCOVIA MUTEMBEI TEMMY
MWOMBAJI: ALISON RICHARD MUTEMBEI NA RICHARD TEMMY BAMWENZAKI
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 01 Mwezi wa Desemba, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10 Mwezi wa Novemba, 2021.**

NAIBU MSAJILI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HIYASINTA ANTONI MALLYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 552 CJG – TOYOTA STARLET.** Chassis namba **EP 910310775.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/CHA/ RB/424640/2021.**

---

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Milipuko miwili yaua, yajeruhi Uganda

**Kampala,** UGANDA

WATU wanne miongoni mwao maofisa wawili wa polisi, wameuawa katika milipuko miwili tofauti katika mji mkuu, Kampala, vyombo vya habari vya ndani vimeripoti.

**Miili miwili imepatikana baada ya mlipuko katika barabara ya bunge katikati mwa Kampala.**

Kwa mujibu wa mashuhuda, mlipuko mmoja ulitokea karibu na kituo cha polisi na mwingine karibu na jengo la bunge.

Shirika la Utangazaji la Uganda (UBC), lilisema baadhi ya wabunge wameonekana wakikimbia nje ya jengo la bunge.

Msaidizi wa Inspekta Jenerali wa Polisi wa Uganda, Edward Ochom, alilieleza shirika la habari la AFP, kwamba hadi sasa wanachoweza kusema, lilikuwa ni shambulio na wanachunguza kubaini wahusika.

Msemaji wa Wizara ya Afya, Ainebyoona Emmanuel, alisema Hospitali ya Mulago iliyopo mjini Kampala, inawahudumia watu 24 waliojeruhiwa, wanne kati yao wako mahututi.

Tovuti inayomilikiwa na serikali ya New Vision ilisema kuwa miili miwili imepatikana katika eneo la mlipuko karibu na jengo la bunge.

"Miili miwili imepatikana baada ya mlipuko katika barabara ya bunge katikati mwa Kampala," ilisema.

Televisheni binafsi ya Urban, inasema maofisa wawili wa polisi walithibitishwa kuuawa katika shambulio tofauti, lililolenga kituo kikuu cha polisi katika mji mkuu.

Tovuti ya Independent, inasema hospitali kuu mjini Kampala imezidiwa na idadi ya waathiriwa wa milipuko hiyo miwili. Milipuko hiyo miwili inafuatia shambulio la bomu la Oktoba 23, katika mgahawa mmoja mjini Kampala, mtu mmoja aliuawa.

Kundi linalojiita Islamic State (IS) baadaye lilidai kufanya shambulizi hilo.

Polisi Uganda wanatumia mbwa wa kunusa kutafuta ushahidi zaidi na kugundua vilipuzi vyovyote kwenye maeneo ya milipuko katikati mwa mji mkuu, Kampala.

Gazeti la Daily Monitor lilichapisha picha za operesheni hiyo.

Meja Jenerali Abel Kandiho, Mkuu wa Ujasusi wa Kijeshi (CMI) na maofisa wengine wa usalama wamefika katika eneo la tukio.

Maofisa wa usalama waliongeza doria katika jiji lote, NTV Uganda iliripoti. Gazeti la Daily Monitor linaripoti kuwa bunge limesitisha vikao vyake.

Wodi ya majeruhi ya hospitali kuu katika mji mkuu wa Uganda, Kampala, imejaa watu waliojeruhiwa katika milipuko ya asubuhi, tovuti ya habari ya Independent inaripoti.

Inasema wengi wa waliojeruhiwa ambao walikuwa wameletwa katika Hospitali ya Mulago kwa magari ya wagonjwa ni maofisa wa polisi.

Kituo cha runinga cha NTV kimezungumza na daktari katika kituo kingine cha afya ambaye alisema walipokea majeruhi 17.

Kumi na wawili walishauriwa kwenda Mulago huku wengine watano wakiruhdishwa nyumbani.

Maofisa wa usalama walikagua majengo ya bunge mjini Kampala, Uganda kufuatia milipuko miwili katikati mwa jiji, ambayo moja ililipuka karibu na bunge. Spika wa Bunge ameahirisha vikao vya jana. Polisi walimwondoa spika na maofisa wengine.

Mwandishi wa habari wa Uganda alituma video ya mbwa wa kunusa kwenye mtandao wa twitter wakiwa ndani ya majengo ya bunge:

Mtu mmoja aliuawa na wengine saba kujeruhiwa katika mlipuko uliotokea mjini Kampala Oktoba 23. Mlipuko mwingine ulitokea siku mbili baadaye katika basi la abiria na kumuua mshambuliaji wa kujitoa muhanga, kwa mujibu wa polisi. **BBC/DW**

## Burkina Faso yaomboleza kitaifa

**Soum,** BURKINA FASO

BURKINA FASO, imetangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa baada ya shambulio lililotokea katika eneo la Inata katika jimbo la Soum Jumapili Novemba 14.

Taarifa iliyotolewa juzi jioni, askari 28 na raia wanne, waliuawa.

"Tunapaswa kuwa na umoja na mshikamano dhidi ya makundi ya kikatili ambayo yanataka kutuingiza katika vita visivyo na huruma, ambavyo lengo lake ni kuwaangamiza raia," Rais wa Burkina Faso alisema Jumatatu, kwenye akaunti yake ya Twitter.

Katika taarifa yake, serikali imethibitisha kuwa takriban watu 32 waliuawa katika shambulio la Jumapili.

Idadi hiyo inaweza kuongezeka, huku walionusurika wakiendelea kutafutwa.

Watu wenye silaha walivamia kikosi cha wanajeshi Novemba 14. Ni moja ya shambulizi baya zaidi kutekelezwa dhidi ya vikosi vya ulinzi na usalama, tangu mashambulizi kuanza nchini humo.

Jeshi la Anga liliitwa kusaidia kurejesha udhibiti wa eneo lililoshambuliwa. Chanzo cha usalama kimesema watu waliotekeleza shambulizi hilo walikuwa hapo kuanzia saa tisa usiku na walikaa hapo hadi saa 12 asubuhi.

Operesheni ya kutafuta watu wanaosadikiwa kutoweka unaendelea. Eneo ambalo shambulio hilo lilifanyika ni kubwa kabisa kwa mujibu wa mamlaka.

Novemba 12, maofisa saba wa polisi waliuawa katika shambulio katika eneo hilo. **RFI**



Wakimbizi waliokusanyika eneo la mpakani mwa Belarusian na Polish wakivuka kuelekea Bruzgi-Kuznica, jana. **PICHA: REUTERS**

## Askari magereza wakamatwa kutoroka kwa wafungwa

**Nairobi,** KENYA

SERIKALI ya Kenya inasema vitengo vya usalama viko katika hali ya tahadhari baada ya kutoroka kwa wafungwa watatu, waliopatikana na hatia ya kuwa magaidi kutoka kwa jela inayolindwa zaidi Kenya.

Mmoja ya waliotoroka alihukumiwa kwa shambulio la 2015 katika chuo kikuu cha Garissa, takribani watu 150 waliuawa. Mwingine alikuwa amepatikana na hatia kwa jaribio lililotibuliwa la bunge la Kenya na wa tatu kwa kuvuka Somalia kujiunga na al-Shabab.

Vitengo vya usalama vimeimarisha usalama katika mipaka ya Kenya huku askari magereza saba waliendа jela, wakikamatwa.

Maofisa wa upelelezi wanachunguza jinsi watu wanaotajwa kuwa hatari zaidi wanaweza kutoroka katika jela ya kamiti. Gereza hilo, linalolindwa zaidi lipo kilomita 20 Kaskazini Mashariki mwa mji mkuu wa Nairobi.

Katika taarifa, Waziri wa masuala ya Ndani, Fred Matiangi, alisema kwamba wachunguzi wanachunguza iwapo wafungwa hao walitoroka kutokana na uzembe au ulegevu wa maofisa. Tayari serikali imetangaza donge nono la dola 550,000 iwapo mtu yeyote atawajulisha polisi walipo watuhumiwa wa tukio hilo. **BBC**

## Jenerali Haftar wa Libya atangaza kuwania urais

**Tripoli,** LIBYA

JENERALI wa Libya, Khalifa Haftar, ambaye jeshi lake liko Mashariki mwa nchi hiyo, ametangaza kuwa ana nia ya kugombea urais katika uchaguzi utakaofanyika mwezi ujao.

Katika hotuba yake kwa njia ya televisheni, Jenerali Haftar amesema uchaguzi ndio njia pekee ya kutoka katika mgogoro mkubwa wa Libya.

Mwendesha mashtaka wa kijeshi, Mohamed Gharouda, tayari aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kukataa uwezekano wa Jenerali Haftar kugombea, kwa sababu ya mashambulizi aliyoanzisha dhidi ya mji mkuu wa Tripoli mwaka 2019. **BBC**

# NCHIMBI BADO MWEZI MMOJA KUSEPA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Ditram Nchimbi, amebakisha mwezi mmoja tu kwenye klabu hiyo kumaliza mkataba wake wa miaka miwili, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa kuondoka kutokana na kukosa namba kwenye kikosi cha kwanza.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema kuwa mkataba wa Nchimbi unamalizika Desemba 15, lakini mpaka sasa wanamhesabia kuwa ni mchezaji wao mpaka pale utakapomalizika, ndipo watatangaza au kuamua vinginevyo.

Bumbuli amekanusha taarifa kuwa mchezaji huyo ameandika barua ya kuomba kuondoka kwenye klabu hiyo, na badala yake amesema kutoonekana kwake kunatokana na kuomba ruhusa kwa sababu ya matatizo ya kifamilia.

"Hakuna barua yoyote aliyoandika, kwa sababu mkataba wake umanalizika tarehe 15 mwezi ujao, na ndicho kipindi pia cha usajili wa dirisha dogo kinaanza, hivyo wala hakuwa na hana sababu yoyote ya kuandika ili aondoke, kwa sababu ikifika muda huo anakuwa huru, hapo anaweza kuondoka, au vinginevyo," alisema Bumbuli.

Kuhusu kutoonekana kwake kwenye mechi mbili za kirafiki ambazo Yanga ilicheza Zanzibar, alisema kumetokana na kuomba likizo fupi ya kushughulikia matatizo ya kifamilia yanayomkabili.

"Hatuwezi kumwita haraka kabla matatizo yake hayajaisha, tunasubiri yaishe na tutakaa na kuzungumza naye, kama tutaendelea naye sawa, lakini kama ikishindikana basi tutamalizana naye kiungwana na ndiyo uungwana wa timu ya Wananchi, ametufanyia kazi nzuri na tutamtakia kila la kheri, lakini mpaka sasa bado ni mchezaji wetu," alisema.

Nchimbi kwa sasa amekuwa siyo sehemu ya kikosi cha kwanza cha timu hiyo kutokana na usajili mkubwa uliofanyika msimu huu.

Nchimbi alisajiliwa Desemba, 2019 kipindi cha dirisha dogo akitokea Polisi Tanzania, alikokuwa akiichezea kwa mkopo akitokea Azam FC.

**TUPO VIZURI...**



Wachezaji wa timu ya Yanga B, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## SGA Security yadhamini tamasha la watoto

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya SGA Security imetangaza kuendelea kukuza vipaji vya vijana wenye umri mdogo kupitia akademi za mpira nchini.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, Eric Sambu, wakati wa tamasha la mpira la siku moja maarufu kama 'All Stars Day' lililoandaliwa na Magnet Youth Academy ya jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Tamasha hilo la kila mwaka, liliwakusanya zaidi ya watoto 300 kutoka akademi zote za Magnet ambapo SGA Security ilikuwa moja ya wadhamini. SGA pia inadhamini timu za mpira za chini ya umri wa miaka 17 na 19 ambazo zinashiriki kwenye Ligi ya Taifa ya Vijana (National Youth League).

Sambu aliipongeza akademi hiyo kwa kukuza vipaji ambapo vijana wengi wamechaguliwa kwenda kwa majaribio akademi kubwa barani Ulaya.

Timu ya wauguzi wa SGA wakiwa na magari ya huduma ya kwanza walishiriki vilivyo katika tamasha hilo kuhakikisha washiriki hawaondoki na majeraha.

"Dira yetu kama SGA ni kutoa huduma za ulinzi, lakini pia tunalipa kipaumbele suala la afya ndio maana tuna magari ya huduma ya kwanza kila kona ya jiji ili kusaidia pale ambapo kuna uhitaji. Matamasha kama haya ya michezo ni kichocheo kikubwa cha afya njema katika nyanja mbalimbali ikiwamo mchezo wa soka," alisema Sambu.

Mwenyekiti wa Magnet Sports Academy, Tuntufye Mwambusi, aliipongeza SGA na kampuni nyingine kwa kuendelea kuchangia tamasha hilo la kila mwaka huku akibainisha kuwa SGA imekuwa mdhamini kwa miaka mitatu sasa.

Alisema akademi yake imezalisha wachezaji katika ngazi mbalimbali za kitaifa. "Wachezaji wetu wana upeo mkubwa kwani wameshiriki katika matamasha makubwa ya mpira nchini Sweden, Norway, Ujerumani na nchi za Kiarabu (UAE). Tumepata pia fursa ya kufundishwa na makocha wazoefu kutoka Hispania na wengi wa wachezaji wetu wameshaenda kwa majaribio barani Ulaya," alisema.

## Mchezaji Dodoma Jiji asajiliwa na Al Hilal

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Dodoma Jiji, David Uromi, amejiunga na klabu ya Al Hilal ya Sudan, huku timu yake hiyo ikimtakia kila la kheri kwenye majukumu yake mpya na kulitangaza vema jina la Tanzania.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Uhusiano ya klabu hiyo, imeeleza imefikia makubaliano na Al Hilal kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo wa zamani wa Ruvu Shooting ambaye pia ana uwezo wa kucheza kama winga wa kulia, ingawa haijaweka wazi dau lililotumika kumng'oa na usajili wake ni wa miaka mingapi.

"Klabu yetu inapenda kuwajulisha wanahabari, mashabiki na wapenzi wa soka kuwa tumefikia makubaliano ya uhamisho wa mchezaji David Uromi kujiunga na Klabu ya Al Hilal, inayoshiriki Ligi Kuu nchini Sudan.

"Klabu yetu inatoa shukrani za kipekee kwa mchezaji Uromi kwa mchango wake mkubwa kwenye timu yetu na tunamtakiwa kila la kheri kwenye majukumu yake mapya," ilieleza taarifa hiyo ya Dodoma Jiji.

Ulomi alisajiliwa na Dodoma Jiji Agosti mwaka huu, akiitumikia timu hiyo kwa kipindi kisichozidi miezi miwili na nusu, akitokea Ruvu Shooting.

## Tanzania Ufukweni kuivaa Msumbiji leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, kimetua salama nchini Afrika Kusini na kesho kitashuka katika Uwanja wa South Beach Arena kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya timu ya Taifa ya Msumbiji kwenye mashindano ya COSAFA, ambayo yalianza jana nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, Boniface Pawasa, alisema kikosi cha wachezaji 14 kimewasili nchini humo salama na wamefanya maandalizi mazuri na wako tayari kwa ajili ya mechi yao hiyo ya kesho dhidi ya Msumbiji.

Alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanapeperusha vema bendera ya Tanzania na ana atarajia kuona wachezaji wake wakipambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Hakuna mashindano rahisi, tuna waheshimu wapinzani wetu na tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata ushindi katika mechi yetu dhidi ya Msumbiji kwa kucheza kwa tahadhari na nidhamu ya hali ya juu," alisema Pawassa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALAH HUYO BARCA

BARCELONA "inafanyia kazi kimya kimya" mpango wa kumvuta mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed, Salah, kumleta Nou Camp, huku kocha mpya Xavi akimtaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 "kwa gharama yoyote". **(El Nacional)**

### CHO KWA CHELSEA, ATLETICO

AC Milan imeungana na Chelsea na Atletico Madrid katika mbio za kumwania mshambuliaji wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya miaka 17, Mohamed-Ali Cho, kutoka Angers. **(L'Equipe)**

### LACAZETTE KUONDOKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, na mshambuliaji wa zamani wa timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, Eddie Nketiah mwenye miaka 22, wanajiandaa kutimka Arsenal mikataba yao itakapomalizika katika majira ya joto. **(Football London)**

### AZPILICUETA NAYE ATAJWA

BARCA wanafuatilia pia suala la Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32 pale Chelsea. Mlinzi huyo Mhispania yuko katika miezi nane ya mwisho ya mkataba wake pale Chelsea. **(ESPN)**

### STERLING HAIWEZEKANI

MPANGO wa Barca wa kumsajili kwa mkopo winga wa England, Raheem Sterling kutoka Manchester City Januari "unaonekana kama si rahisi" kwa sababu ya hali yao kifedha na mshahara wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 26. **(Sport)**

### KULUSEVSKI KUBADILISHWA NA PEPE

JUVENTUS wanataka kumwondoa winga wake raia wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 21, huku kukipendekezwa mpango wa kubadilishana na Arsenal ili wamchukue winga wao kutoka Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26. **(Calciomercato)**

### TCHOUAMENI ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United inamtaka kiungo wa Monaco na Ufaransa Aurelien Tchouameni, 21, ambaye pia anasakwa na klabu za Chelsea, Liverpool, Manchester City, Real Madrid, Paris St-Germain na Bayern Munich. **(El Nacional, via Sun)**

### VILLA WAMTAKA PATTERSON

ASTON Villa wanamtaka mlinzi wa Rangers, Nathan Patterson kutokana na ujio wa Steven Gerrard kama kocha wao mpya akitokea kwa mabingwa hao wa Scotland, Rangers. **(90min)**

### NUNO KWENDA UFARANSA

NUNO Espirito Santo anataka kurejea kufundisha haraka katika Ligi Kuu England baada ya kutimuliwa Tottenham, lakini wakala wake anaangalia uwezekano wa kocha huyo kwenda Ufaransa huku timu za Lyon na Lille zikionekana kituo kinachoweza kufuata kwake. **(Sun)**

### SWIFT AGOMBEWA ENGLAND

LEEDS United, Wolves na Burnley zinamnyatia kiungo wa Reading na mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, John Swift mwenye umri wa miaka 26. **(Sheffield Star)**

### JESSE MAMBO SAFI

NEWCASTLE United wanamatumaini kwamba fursa ya kuanza kikosi cha kwanza kutaongeza nafasi yao ya kumsajili kiungo wa England, Jesse Lingard mwenye miaka 28, kutoka Manchester United Januari. **(Northern Echo)**

### DE VRIJ KUONDOKA INTER

MLINZI wa Uholanzi, Stefan de Vrij mwenye miaka 29, amewaambia marafiki zake anataka kuondoka Inter Milan kujiunga na Tottenham Januari. **(Football Insider)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE AJIWEKEA REKODI ENGLAND IKIFUZU QATAR

Amefunga mabao manne wakati wakiiadhibu San Marino 9-0 na kuweka historia baada ya…

**LONDON, England**

NAHODHA wa England, Harry Kane ameweka rekodi mpya kwa 'Simba Watatu' hao kwa kufunga bao lake la 13 kwa kalenda ya mwaka mmoja 2021 dhidi ya San Marino, Jumanne.

Kane kwenye mchezo huo alifunga mabao manne wakati England ikiiadhibu San Marino mabao 9-0.

George Hilsdon (mwaka 1908) na Dixie Dean (mwaka 1927) kwa muda mrefu walishikilia rekodi ya kuifungia mabao 12 timu ya Taifa ya England kwa mwaka mmoja, kabla ya Kane kuifikia mwaka 2019.

Mshambuliaji huyo wa Tottenham Hotspur aliifikia tena rekodi hiyo wakati akifunga mabao matatu dhidi ya Albania Ijumaa sambamba na hat-trick yake ya nne ya kimataifa.

Ushindi wa mabao 5-0 pale kwenye dimba la Wembley ulimaanisha kwamba, England walikuwa wakihitaji pointi moja tu dhidi ya San Marino ili kufuzu kushiriki michuano ya Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.

"(Kane) ni mchezaji mwenye haraka na mwepesi, hivyo kufunga kwake ni jambo la kawaida," alisema kocha wa England, Gareth Southgate baada ya mchezo huo.

Katika mchezo huo wa Jumatatu, Kikosi cha England pia kilishuhudiwa kutolewa nafasi kwa Emile Smith Rowe, ambaye alifunga bao akiwa mmoja wa wachezaji wasio wazoefu.

Kane katika mchezo huo alifunga mabao manne akiaanza kwa la tatu kwa penalti katika dakika ya 27 baada ya Harry Maguire kuanza kufunga la kwanza na Filippo Fabbri kujifunga.

MECHI KALI
HOME
AWAY
STOCKPORT
3.21 | 3.56 | 2.07
BOLTON
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS.686



# LUKAKU AANZA MAZOEZI CHELSEA

**LONDON, England**

ROMELU Lukaku amerudi kwenye mazoezi Jumatatu katika kikosi cha Chelsea ikiwa ni baada ya kukosa mechi tano kutokana na kuumia kifundo cha mguu.

Lukaku mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, alilazimika kutolewa nje dakika ya 23 wakati Chelsea ikishinda mabao 4-0 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Malmo Oktoba 20 baada ya kukwatuliwa na Lasse Nielsen.

Timo Werner pia aliumia misuli kwenye mchezo huo na amekuwa nje tangu wakati huo, lakini Chelsea walicheza mechi tatu bila kupoteza kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

'Blues' hao walikuwa na wastani wa mabao 2.6 kwa mchezo.

Katika mechi zao nane za mashindano yote msimu huu wakati Lukaku na Werner wakiwamo kikosini, Blues walikuwa na wastani wa mabao 2.1.

Hata hivyo, mabao 11 kwenye ligi ya Chelsea, yalifungwa wakati wawili hao wakiwamo uwanjani.

Kuna matumaini kwamba, Lukaku, ambaye hajafunga kwa kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel tangu Septemba, anaweza kuanza kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Leicester City Jumamosi.

Marcos Alonso pia alianza mazoezi Jumatatu hiyo, ikiwa ni baada ya kukaa nje kwenye sare dhidi ya Burnley kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa kwa tatizo la kifundo cha mguu.

# Mancini na imani Italia kufuzu Qatar



**ROME, Italia**

ROBERTO Mancini ana "imani kubwa" Italia itafuzu kwenye michuano ya Kombe la Dunia Qatar 2022, baada ya sare ya bila kufunga na Ireland Kaskazini kuwafanya washindwe kufuzu moja kwa moja.

Mabingwa hao wa Ulaya 2020, walikwenda kwenye mchezo wao wa mwisho wa Kundi C pale kwenye dimba la Windsor Park Jumatatu wakiwa kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya mabao na Uswisi.

Lakini Ireland Kaskazini ilionekana kama imewasaidia Uswisi kufuzu, baada ya 'Azzurri' kushinda kupata ushindi huku golikipa Bailey Peacock-Farrell akiibuka shujaa kwa kuzuia mashuti ya Italia.

Uswisi hawakuwa na tabu hiyo, kwani wao walifunga Bulgaria mabao 4-0 na kupaa kileleni mwa msimamo na hivyo kufuzu moja kwa moja kwenye michuano hiyo mwakani.

Azzurri sasa lazima washinde mchezo wa mtoano wa timu zilizoshika nafasi ya pili ili wapate nafasi ya kufuzu kwenda kwenye michuano hiyo mikubwa zaidi duniani huku wao wakiwa moja ya timu zilizotwaa kombe hilo mara nyingi zaidi.

Italia imetwaa mara nne Kombe la Dunia sawa na Ujerumani, wakiongozwa na Brazil iliyolibeba mara tano.

Michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2018, Italia walishindwa kufuzu, lakini wakaamkia kwenye mashindano ya Euro 2020 ambapo walitwaa kombe hilo.

Baada ya mchezo huo, Mancini aliwaambia waandishi wa habari: "Licha ya kutawala mchezo, tulishindwa kufunga mabao na hilo kwa sasa naliona kama tatizo.

"Tulihitaji kufunga mapema, lakini tulishindwa. Ni aibu kwa sababu tulitakiwa kumaliza mambo kwa urahisi tu katika kundi hili.

"Lakini nina imani kubwa tuna nafasi kubwa ya kufuzu kwenye mechi za mtoano kwa washindi wa pili Machi mwakani."

**HABARI MICHEZO**

# 6,934,380 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20.11.21 | 18:00 | Burnley vs Crystal Palace | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 2. 20.11.21 | 18:00 | Aston Villa vs Brighton | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 3. 20.11.21 | 18:00 | Newcastle vs Brentford | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 4.20.11.21 | 18:00 | Wolverhampton vs West Ham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 5. 20.11.21 | 18:00 | Hull City vs Birmingham | 2.63 | 3.12 | 2.63 |
| 6. 20.11.21 | 18:00 | Reading vs Nottingham | 2.89 | 3.18 | 2.39 |
| 7. 20.11.21 | 20:00 | Lazio vs Juventus | 2.78 | 3.36 | 2.48 |
| 8. 20.11.21 | 20:45 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 9. 20.11.21 | 22:45 | Fiorentina vs AC Milan | 3.09 | 3.39 | 2.26 |
| 10. 21.11.21 | 15:00 | Brest vs Lens | 3.03 | 3.43 | 2.26 |
| 11. 21.11.21 | 17:00 | Salernitana vs Sampdoria | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 12. 21.11.21 | 17:00 | Troyes vs St Etienne | 2.35 | 3.34 | 2.94 |
| 13. 21.11.21 | 17:00 | Metz vs Bordeaux | 2.42 | 3.28 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 17 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2374 | Junior Sevan vs Alashkert Martuni | 2.55 | 2.98 | 2.69 |
| 13:30 | 5198 | Levski 2005 Krumovgrad vs Montana | 2.85 | 3.33 | 2.23 |
| 13:30 | 5986 | AD Alcorcon B vs Alcobendas Sport | 2.60 | 3.03 | 2.60 |
| 14:00 | 2192 | FC Olimp Dolgoprudny vs Torpedo Moscow | 3.86 | 3.28 | 1.86 |
| 14:00 | 5123 | Gazovik Orenburg vs Tom Tomsk | 1.33 | 4.54 | 7.73 |
| 15:00 | 1334 | Czarni Sosnowiec W vs Gornik Leczna W | 1.80 | 3.80 | 3.56 |
| 15:00 | 1629 | Stropkov vs FK Puchov | 2.84 | 3.61 | 2.12 |
| 15:00 | 2508 | Nong Bua Pitchaya vs Bangkok Glass | 3.95 | 3.32 | 1.83 |
| 15:00 | 5456 | Yenisey Kr vs Tekstilshchik | 1.42 | 4.16 | 6.39 |
| 16:00 | 1508 | FC Rotor Volgograd vs Metalurg Lypetsk | 1.35 | 4.52 | 7.31 |
| 17:00 | 3116 | Neftekhimik vs Baltika Kaliningrad | 2.39 | 3.09 | 2.80 |
| 17:30 | 2482 | Urartu vs Bkma Yerevan | 1.16 | 5.94 | 14.38 |
| 18:00 | 3347 | Urozhay Krasnodar vs FC Alania Vladikavkaz | 3.51 | 3.42 | 1.91 |
| 18:00 | 4248 | FC Krasnodar II vs Ska Energiya | 2.74 | 3.13 | 2.41 |
| 18:00 | 4491 | Akron Tolyatti vs Fakel | 4.34 | 3.52 | 1.71 |
| 18:00 | 5897 | KamAZ vs Volgar Astrahan | 2.10 | 3.13 | 3.28 |
| 18:30 | 2981 | Veles vs Spartak II Moscow | 1.87 | 3.52 | 3.56 |
| 18:30 | 3032 | Pinatar Arena FC vs CF Castillo Huercal Overa | 2.03 | 3.27 | 3.32 |
| 20:00 | 1436 | Sandecja vs Skra Czestochowa | 1.81 | 3.52 | 3.81 |
| 20:00 | 1438 | CF Getafe B vs AD Complutense Alcala | 1.62 | 3.43 | 5.21 |
| 20:00 | 2443 | Union Viera CF vs CD Vera | 3.05 | 3.15 | 2.39 |
| 20:00 | 2891 | Atletico Madrid B vs Carabanchel | 1.29 | 4.55 | 9.68 |
| 20:00 | 3309 | JK Tammeka Tartu II vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.91 | 4.25 | 3.21 |
| 20:45 | 5406 | Kopparbergs Go W vs SL Benfica W | 1.69 | 3.85 | 4.05 |
| 21:00 | 1091 | Carl Zeiss Jena vs VfB Auerbach | 1.36 | 4.72 | 6.56 |
| 21:30 | 2902 | Taftea IK vs Skellefteaa FF | 3.95 | 3.80 | 1.71 |
| 21:30 | 4459 | Sandvikens AIK FK vs FC Stockholm Internazionale | 13.53 | 7.92 | 1.11 |
| 22:00 | 1371 | CD Galapagar vs CF Pozuelo De Alarcon | 3.15 | 3.15 | 2.34 |
| 22:00 | 2091 | CF Fuenlabrada B vs ED Moratalaz | 1.98 | 3.35 | 3.90 |
| 22:00 | 3502 | CDF Tres Cantos vs RSD Alcala | 3.18 | 2.98 | 2.22 |
| 22:00 | 4845 | AD Parla vs AD Villaviciosa | 1.59 | 3.77 | 4.83 |
| 22:30 | 1057 | AD Torrejon CF vs Colonia Moscardo | 1.56 | 3.66 | 5.39 |
| 22:30 | 1199 | LAS Rozas vs Rayo Vallecano B | 2.22 | 3.30 | 3.30 |
| 22:30 | 2915 | Trival Valderas A. vs Villaverde Boetticher | 1.74 | 3.50 | 5.00 |
| 22:45 | 1226 | Stockport vs Bolton | 3.21 | 3.56 | 2.07 |
| 22:45 | 5567 | Gosport Borough vs Kings Langley | 1.50 | 4.14 | 5.20 |
| 23:00 | 1826 | Bayern Munich W vs Lyon W | 3.27 | 3.71 | 1.91 |
| **ALHAMISI - 18 - NOVEMBA 2021** | | | | | |
| 00:15 | 3537 | CD Municipal Limeno vs Jocoro FC | 8.40 | 5.00 | 1.35 |
| 00:30 | 2451 | CD FAS vs Chalatenango | 1.68 | 3.56 | 4.43 |
| 01:00 | 2394 | America Mineiro MG vs Atletico GO | 1.65 | 3.42 | 5.01 |
| 01:00 | 4098 | Cuiaba MT vs Internacional | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 01:00 | 4239 | Santos vs Chapecoense | 1.37 | 4.25 | 7.35 |
| 02:00 | 4766 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.06 | 3.08 | 3.46 |
| 02:00 | 4817 | Bogota FC vs Union Magdalena SM | 2.23 | 3.22 | 2.93 |
| 02:30 | 2666 | Juventude RS vs Fluminense | 2.56 | 2.80 | 2.85 |
| 02:30 | 3404 | Palmeiras vs Sao Paulo | 1.92 | 3.18 | 3.80 |
| 03:30 | 4710 | Flamengo vs Corinthians | 1.49 | 3.80 | 5.97 |
| 04:05 | 2104 | Junior Barranquilla vs La Equidad | 1.50 | 3.75 | 5.97 |
| 10:30 | 2527 | Henan Jianye W vs Beijing Baxy W | 2.99 | 3.66 | 2.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ALVES: NAJISIKIA SHUJAA KUVAA JEZI YA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

DANI Alves amesema kuvaa jezi ya Barcelona kunamfanya kujihisi kama "shujaa" baada ya kurudi pale Camp Nou akijaribu "kuiokoa" klabu hiyo.

Alves anarudi kwa miamba hao wa LaLiga kwa mara ya pili baada ya kuondoka kwenda nyumbani kwako Brazil kuichezea klabu ya Sao Paulo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, beki wa pembeni ambaye amesaini mkataba utakaomweka hadi mwishoni mwa msimu huu, hataruhusiwa kucheza hadi Januari.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka Barcelona miaka mitano iliyopita akiwa ameichezea mechi 247 tangu alipotua hapo akitokea Sevilla mwaka 2008.

Alishinda mataji sita ya LaLiga na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya makombe 23 aliyobeba akiwa hapo.

"Kuna jezi mbili nikivaa najisikia kama shujaa: Jezi ya Brazil na Barcelona," alisema Alves akiiambia Barca TV.

"Kwa kuvaa jezi hii, kwa hakika kabisa, najiona mimi ni shujaa na nimekuja hapa kuimarisha klabu."

# Tchouameni agombewa Chelsea, Madrid



**LONDON, England**

KIUNGO wa Monaco, Aurelien Tchouameni, anazivutia klabu mbalimbali barani Ulaya baada ya kuonyesha kiwango bora ndani ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, pamoja na kufanikiwa kuitwa katika Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Klabu ya Real Madrid ni miongoni mwa zilizoonyesha nia ya kutaka kupata huduma ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Lakini si wao pekee yao waliona kipaji cha kiungo huyo bali Chelsea pia wanamtolea macho Tchouameni na wamemweka katika orodha ya wachezaji wanaotakiwa kutua darajani.

Na klabu hiyo ya Ligi Kuu England ndio wagombea wakuu na wanatarajia mchezaji huyo wa Monaco kuhamia 'The Blues' majira ya joto yanayokuja.

Kwa mujibu wa Transfermarkt, kinda huyo anaweza kupanda thamani kutoka euro milioni 18 mpaka euro milioni 36 tangu kuanza kwa msimu huu.

Michezo

Jumatano Novemba 17, 2021

Nipashe



## Kane aweka rekodi England ikifuzu Qatar

UKURASA 21

# PABLO ADUWAZA UFUNDI SIMBA

## ●●●Sasa ni ‘mpera mpera’ tu, wachezaji ni kugusa, kuachia na kufungua, uongozi wataja sababu kumleta Castro...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU uongozi wa Klabu ya Simba ukieleza sababu ya kumleta fundi mwingine, Don Daniel de Castro kutoka nchini Hispania, ambaye ni kocha wa viungo, huko mazoezini unaambiwa ni mwendo wa ‘mpera mpera’ (kasi ya ajabu), anayoitaka Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mhispania Pablo Franco wakati wachezaji wakiwa na mpira na wanapoteza.

Simba juzi ilimtangaza kocha mpya wa viungo, De Castro kutoka Hispania, ambaye ameungana na Kocha Mkuu Mhispania mwenzake, Franco aliyejiunga na kuanza kazi hivi karibuni.

Hata hivyo, katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea Uwanja wa Boko Veterans, Dar es Salaam, Franco ameanza kukibadilisha kikosi hicho kwa kutaka mchezo wa pasi za haraka na kasi kwa wachezaji.

Franco anaonekana kuwa muumini wa pasi za haraka kwani katika mazoezi hayo, amekuwa akiwataka wachezaji kugusa mpira mara moja na kuachia kisha kukimbia mbele kufungua vyumba, lakini pia akiwazuia kupiga pasi za nyuma (back pass).

Mbinu nyingine ambayo Franco anaonekana kuitumia ni wachezaji kukabia juu ya mstari na nyuma wakibaki mabeki watatu.

Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, tayari amekiri si wachezaji tu wananufaika na mbinu za kocha huyo bali hata yeye kuna vitu vingi vipya ameanza kujifunza kutoka kwa Franco.

Hitimana amesema kuna mambo mengi mapya anayapata kutoka kwa kocha huyo na anaamini ni muda tu unahitajika kabla ya mashabiki kushuhudia mabadiliko makubwa katika kikosi chao.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema Castro, aliyetua kuchukua mikoba ya Adel Zrane raia wa Tunisia aliyeondolewa hivi karibuni, wamemchukua kwa sababu ya kukidhi matarajio ya klabu, lakini pia ni masharti yaliyowekwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na la Tanzania (TFF).

“Tumemchukua kwa sababu ya kukidhi matarajio ya klabu yetu, tumeona atatufaa, lakini kikubwa ni masharti ya CAF na TFF wanaotaka wataalamu hao ni lazima wafike viwango fulani, kwa hiyo sisi pamoja na kwamba tumeridhika naye, pia vigezo vyake vinakidhi na kukubaliana na masharti yaliowekwa na wanaoongoza soka,” alisema Mangungu.

Elimu ya Castro ni shahada ya utaalamu wa elimu ya mwili (UEFA-A) aliyoipata katika Chuo cha Laguna, Hispania mwaka 2010, huku pia akiwa na shahada ya mafunzo ya utimamu wa mwili katika soka aliyoipata 2018/19 kwenye chuo cha Madrid.

Pia amefanya kozi ya mafunzo ya uchambuzi wa viwango katika soka kutoka Chuo Kikuu cha Plytechnic Madrid mwaka 2018.

Kuhusu wasifu wa kocha huyo, msimu wa 2018 alikuwa kocha msaidizi wa Real Madrid wa vijana chini ya miaka 18 ambayo ilitwaa ubingwa wa Hispania, msimu wa 2020/21 alikuwa kocha msaidizi wa viungo wa timu ya Politehnica ya Romania na 2019/20 alikuwa kocha msaidizi wa viungo wa timu ya Rapid Bucharest ya Romania pia.




Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco.

## Namungo yaanika pakupenya Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco amesema wanaendelea vizuri na maandalizi na wanatambua Yanga wako vizuri, lakini hawajawa kamili kwa asilimia 100, hivyo watatumia udhaifu huo kupata pointi tatu katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo FC watakuwa wenyeji katika mchezo huo wa raundi ya sita utakaopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Morocco alisema amepata bahati ya kuiona Yanga inapocheza na wamekuwa na matokeo mazuri katika michezo mitano waliyocheza tofauti na wao ambao hawakuanza vizuri.

Alisema mbali na kutoanza vizuri katika ligi hiyo na ubora wa wapinzani wao, wataingia uwanjani kuwaheshimu na kutumia udhaifu wa Yanga kutafuta pointi muhimu katika uwanja wa nyumbani katika mechi hiyo.

“Yanga imeanza vizuri na kuonekana bora, ukiangalia kiufundi hawajakamilika kwa asilimia zote, wanaupungufu ambao tutautumia kutafuta matokeo chanya ili kuondoka na pointi tatu katika mchezo huo,” alisema Morocco.

Alisema wanaiheshimu Yanga, lakini hawataiogopa na anatarajia mchezo huo utakuwa mzuri kwa sababu ya aina ya wachezaji walikuwa nao.

“Hatuwezi kuweka silaha zetu kwa wapinzani wetu, ila tunaingia kwa staili nyingine na mbinu tofauti na mechi tano tulizocheza. Tumejiimarisha kila idara na hatutowapa nafasi washambuliaji wa wapinzani kuleta madhara katika eneo letu ili kuhakikisha tunapata pointi tatu katika mchezo huo na kujiweka sehemu salama katika msimamo,” alisema Morocco.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042